epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Ijumaa Juni 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581700

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**NEYMAR AMPA VINICIUS BALLON D'OR**



## MIKOPO HESLB

# Hesabu yake yazua utata

UKURASA 2

**BIL 787/-**
Fungu lililotengwa kwa ajili ya mikopo mwaka 2024/25

**250,000**
Idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kunufaika

**MIL 3.148/-**
Wastani wa kiasi ambacho kila mnufaika atakopeshwa

**MIL 2.4/-**
Kiasi anachokopeshwa mnufaika kama posho ya kujikimu 'boom'

UKURASA WA 2

**NCHIMBI AONYA SIASA ZA KUNOA MAPANGA, VISU UCHAGUZI UJAO**

UKURASA WA 4

**WAZIRI MKUMBO: WAKOREA KUFURIKA KUWEKEZA TANZANIA**

UKURASA WA 4

**MAHAKAMA YABARIKI BODABODA ANYONGWE**

## Tani 60,000 za mahindi kuwapa wakulima bilioni 57.148/-

UKURASA 8



Rais Samia Suluhu Hassan akionyesha nakala za kitabu cha 'A Taste of East Africa' baada ya kukizindua wakati wa mkutano na Watanzania waishio Jamhuri ya Korea juzi. Kushoto ni Mwandishi wa Kitabu hicho, Chaba Mavura. **PICHA: IKULU**

# Sheria Ardhi, Uhamiaji kufumuliwa kuwavuta Watanzania wa ughaibuni

UK.3

**MICHEZO** **AZIZ KI AENDELEZA SINTOFAHAMU YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi (katikati) na Naibu Waziri Madini, Dk. Steven Kiruswa, Bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# MIKOPO YA HESLB: Hesabu yazua utata

**Na Pilly Kigome**

DIRISHA la uombaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2024/25 limefunguliwa rasmi, serikali ikitarajia kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 787 kwa wanafunzi 250,000.

Hilo ni ongezeko la wanafunzi 25,944 kulinganishwa na wanufaika 224,056 wa mikopo hiyo kwa mwaka wa masomo 2023/24.

Hata hivyo, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya utoaji mikopo hiyo kinazua utata na kutoa ishara kwamba wanufaika wengi hawatopewa mkopo kwa asilimia 100.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dk. Bill Kiwia, jana alitangaza kufunguliwa dirisha hilo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Dk. Kiwia alisema dirisha la maombi hayo ya mikopo lilifunguliwa rasmi Juni Mosi mwaka huu na litafungwa Agosti 31 mwaka huu, hivyo kuwapo siku 92 kwa ajili ya waombaji mikopo.

Alisema serikali imetenga bajeti ya Sh. bilioni 787 kwa ajili ya ruzuku kwa wanafunzi 250,000, akisisitiza waombaji wahakikishe wanatimiza wajibu kwa kusoma miongozo iliyotolewa na kuzingatia wakati wa kuomba mkopo.

Katika lugha ya hisabati, Sh. bilioni 787 zilizotengwa na serikali kwa ajili ya mikopo kwa wanufaika 250,000 zina maana kutatolewa mkopo wa wastani wa Sh. milioni 3.148 kwa kila mnufaika.

Ni wastani unaotoa ishara kwamba wanafunzi wengi hawatapewa mkopo kwa asilimia 100 kwa kuwa fedha kwa ajili ya kujikimu ni Sh. milioni 2.4 kwa mwaka (Sh. 10,000 kwa siku).

Ukitoa Sh. milioni 2.4 katika fungu la wastani wa Sh. milioni 3.148 kwa kila mnufaika, kitabaki kiasi cha Sh. 748,000 ambacho ndicho mwanachuo atalazimika kukitumia kama kianzio kulipa ada ya chuo, mafunzo kwa vitendo (PT), utafiti, vitabu na vifaa vingine vya darasani.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jana, Dk. Kiwia alisema maombi ya mkopo yatafanywa kwa njia ya mtandao, mwombaji akiwa na nyaraka zote muhimu zilizoainishwa katika miongozo iliyotolewa.

Alisema kuwa Mei 27, mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alizindua miongozo mitano ya utoaji mikopo na ruzuku kwa mwaka wa masomo 2024/25 ambao utaanza mwezi Oktoba mwaka huu.

Uzinduzi huo ulifanywa katika Shule ya Sekondari Popatial, mkoani Tanga. Miongozi hiyo pamoja na ya Utoaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Shahada ya Awali (Bachelor) kwa 2024/25 na wa Utoaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Stashahada (Diploma).

Mingine ni ya Utoaji wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Stashahada ya Umahiri katika Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo kwa Mwaka 2024/25; Utoaji Mikopo kwa Shahada za Umahiri na Uzamivu; na wa Utoaji Ruzuku za Samia kwa Mwaka 2024/25.

Mkurugenzi Mtendaji Kiwia alisema miongozo hiyo imo katika tovuti rasmi ya HESLB kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza ili wadau, wakiwamo wanafunzi, wazazi na walezi, waweze kuisoma na kuielewa vyema.

**HATUA ZA MAOMBI**

Dk. Kiwia alisema mwombaji mkopo anapaswa kuingia katika tovuti rasmi ya HESLB na kubofya sehemu ya kuomba mkopo, atajisajili huko kwa kutumia namba yake ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne na atumie namba ya NIDA kama anayo - kama hana, ataruhusiwa kuendelea na maombi.

"Mwombaji mkopo yeyote atapaswa kuwa na akaunti ya benki aliyofungua katika benki aipendayo. Ni muhimu mwombaji mkopo ahakikishe majina yanayosomeka katika akaunti ya benki yanafafana na yaliyoko katika namba yake ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne," alisema.

# Nchimbi aonya siasa za kunoa visu, mapanga uchaguzi ujao

**Na Romana Mallya,** HIMO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ameonya watu wanaotumia majukwaa ya kisiasa kuhamasisha umwagaji damu kwa kutaka waandae visu, mapanga na majembe kwa ajili ya uchaguzi ujao.

Amewataka Watanzania kuwapima vizuri viongozi wao ili kabla ya kuwapa nafasi, wasipande mbegu ya mauaji katika nchi na kuonya kwamba ikitokea kiongozi wa CCM anachochea watu kuandaa mauaji, atafukuzwa mara moja.

Akizungumza jana na wananchi eneo la Himo Njiapanda, Moshi mkoani Kilimanjaro wakati wa ziara yake ya kutembelea mikoa mitano, alisema jana (juzi) alikuwa akisikiliza habari kwenye mitandao kuhusu mambo yaliyojiri kwenye mikutano ya vyama vya siasa.

Dk. Nchimbi alisema amemsikia kiongozi wa dini ambaye alikuwa mwalikwa kwenye mkutano wa chama cha siasa akiomba wananchi waanze kuandaa visu, mapanga na majembe kwa ajili ya uchaguzi ujao.

"Amesema matumizi yake hayatakuwa matumizi waliyozoea. Hatua moja huanzisha nyingine. Watu ambao wanatamani nchi imwage damu wanaanza kidogo kidogo kutengeneza mazingira ya watu kuuana na wao kuona ni jambo la kawaida.

"Haiwezekani mtu una akili timamu unapanda kwenye mkutano unawaambia watu wafanye maandalizi ya kuuana. Nimemsikiliza yule kiongozi halafu nikasikiliza waliokaa kwenye meza kuu, ndio wanaoongoza kumpiga makofi, kumbe ndio sera ya chama chao.

"Huko ndiko wanataka kutupeleka? Miaka 20 toka tumeingia kwenye mfumo wa vyama vingi bado vyama vya upinzani havitaki kukomaa. Havitaki kujua kwamba kuwa kiongozi maana yake ni kujali maisha ya watu?" alihoji.

Balozi Nchimbi alisema ikitokea kiongozi wa CCM anachochea watu kuandaa mauaji watamfukuza siku hiyo hiyo.

"Ukishaongea maneno ya namna hiyo, kwa kweli ukifanyiwa uchunguzi ni lazima utakutwa umeshafanya mauaji mengi huko nyuma. Umejificha bado una hamu ya kuona watu wanaendelea kufa au una tatizo kubwa la ugonjwa wa akili," alibainisha.

Aliwaomba Watanzania wasifanye masihara katika kuwapima viongozi wao, wahakikishe wanawapima vizuri ili kabla ya kuwapa nafasi wasipande mbegu ya mauaji katika nchi.

"Hayo mambo wanaongea kirahisi rahisi tu, juzi nikiongea na Mkuu wa Wilaya pale Arusha, alinieleza wakati wa mauaji Congo, akasema jambo ambalo hawezi kulisahau ni yeye kushuhudia wanawake saba na wanaume watatu wamekatwa vichwa na kutenganishwa na viwiliwili mbele ya macho yake.

"Haya ndiyo mambo tunataka kuyaleta hapa? "Ninawaomba tuyakatae. Tuwapime watu kwa hoja zao. Hata wale wa upinzani mkae nao wakati mwingine mkizungumza kwa upendo kwamba fanyeni siasa ambazo zinaimarisha upendo na umoja katika nchi," alisisitiza.

Balozi Nchimbi aliomba Watanzania watambue kila mmoja kwenye nafasi yake ana dhamana ya kipekee kuhakikisha nchi inabaki kwenye utulivu na kuendelea kuwa na umoja na serikali ikifanya jitihada za kushajihisha maendeleo.

Kuhusu malalamiko ya mwananchi ambaye ametoa taarifa za wizi wa fedha za serikali katika kijiji chake na sasa kukatazwa kuzungumza chochote cha CCM wala kuingia katika vikao huku Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ikifanya uchunguzi wa fedha hizo, Balozi Nchimbi alisema kila anayetoa taarifa za wizi katika eneo ni mzuri na kutaka chama kimlinde.

**MAUAJI HIFADHINI**

Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, alisema juzi aliuawa kijana mmoja na askari wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA).

"Tunafahamu lazima misitu ya hifadhi ilindwe na tunazingatia hilo, lakini ninaomba kwamba wizara, TAWA (Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania) na TFS (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania).

"Tujaribu kuwaambia wawe na utu waelewe, mtu anakata majani pembeni kwa sababu ng'ombe au mbuzi anakufa njaa pembeni kabisa mwa hifadhi, kumpiga risasi mtu hana silaha inakuwa kama si sawa," alisema.

Akitolea ufafanuzi suala hilo, Balozi Nchimbi alisema wanaunga mkono sheria zinazolinda hifadhi ya misitu, lakini ametaka wakumbuke uhai wa binadamu ni kitu cha kwanza.

"Tunaomba wajali maisha ya watu wetu, kutumia silaha nzito kwa wananchi wasio na silaha si busara, ni jambo la ovyo, ninaielekeza serikali kuhakikisha ubinadamu unatumika katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Ndiyo maana hata sheria inasema lazima kutumia ngumu inayohitajika si kila mahali unatumia nguvu, hakuna sababu, haya ndiyo maelekezo rasmi kwa serikali kutumia busara tunaposhughulikia kesi zinazohusu wananchi," alisema.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, CPA Amos Makalla, akisoma baadhi ya mabango ya wananchi, alisema kuna Kikundi cha Upendo Kahe ambacho tangu mwaka 2020 kimepanda miti 5,000 maeneo tofauti yakiwamo shuleni na vituo vya afya na kuomba ufadhili ili kuzalisha miti mingi zaidi, ombi ambalo Balozi Nchimbi aliwaahidi kuwachangia Sh. milioni mbili.

HABARI KITAIFA

# Sheria za Ardhi, Uhamiaji kufumuliwa

## -Kutoa nafasi diaspora kuwekeza nyumbani

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa** KOREA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema sheria ya ardhi na uhamiaji zitafanyiwa marekebisho ili kutoa nafasi kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi wapate ardhi na kuiendeleza na Sheria ya Uhamiaji ili waliobaki na utanzania na kuishi nje au kuchukua uraia mwingine waweze kurudi nyumbani bila masharti magumu ya visa.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Seoul, Jamhuri ya Korea wakati akizungumza na Diaspora wanaoishi nchini Korea ikiwa ni katika kuhitimisha ziara yake ya siku sita nchini humo kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo na kuhudhuria mkutano wa Korea-Afrika Summit 2024.

Alisema sera ya diaspora imekamilika na imewatambua Watanzania waliopo nje kwa mafungu mawili ya waliobakia na utanzania wao, lakini wanaishi nje na walioacha uraia wao na wamechukua uraia mwingine na ni wazaliwa wa Tanzania.

"Katika sheria ya hadhi maalum ya diaspora makundi hayo yana hadhi tofauti, Mtanzania aliyebaki na utanzania wake ana yake atakayopata na ambaye ana uraia wa nchi nyingine, lakini tumemzaa wenyewe naye ana yake atakayopata," alisema.

"Kuna mchango mkubwa wa diaspora duniani unaokuja nyumbani. Tunajenga nyumba za kisasa ambazo diaspora wamejitokeza kununua. Katika mwaka 2023 Diaspora wengi wamewekeza sekta ya nyumba ambayo imepokea Sh. bilioni 280 ikiwa ni ongezeko la kutoka milioni 800, na uwekezaji kwenye mifuko umeongezeka na kwenye UTT kuna bilioni 6.4 za diaspora," alisema.

Alisema Tanzania kuongezewa mkopo ambao utalipwa kwa miaka 25 kwa riba ya asilimia 0.01 ni kutokana kusimamia vyema mikopo ya awali ikiwamo uliojenga daraja la Tanzanite, kilimo na umwagiliaji na kwamba walivyotajiwa kiwango hicho walishangaa kwa kuwa ni mafanikio makubwa, awali nchi ilikuwa inapewa Dola bilioni moja pekee.

Aidha, Rais Samia alisema amekutana na kampuni mbalimbali ikiwamo ya Samsung na kuwaomba kuja kuwekeza nyumbani ili kutoa ajira za moja kwa moja na manufaa mengi.

"Kuna mafanikio makubwa na kuna dalili nzuri ya kutoa fedha na tufanyakazi nao zaidi. Tumewavutia sekta binafsi ya Korea ije nchini kwenye miundombinu ya reli, barabara na madini. Nimeongea na Rais wa Korea kafurahi sana na yupo tayari kushirikiana nasi," alisema.

Pia Rais Samia alisema lengo la kuambatana na vijana wajasiriamali wakati ambao wanaweza kuwa na kampuni kubwa ni kujifunza na kila ziara atahakikisha anakuwa nao ili wajifunze na kujifunza yanayofaa kuleta nchini.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, January Makamba, alisema ziara hiyo ni ya kihistoria yenye heshima kwa nchi na kwamba tangu uhuru ushirikiano wa kimataifa umekuwa kipaumbele.

"Kutokana na matendo yako ndani ya miaka mitatu ya uongozi, maneno yako, mafanikio ya serikali yako, haiba yako nchi yetu sasa huko duniani inaaminika na kuaminiwa, inaheshimika na kuheshimiwa na inasifika na kusifiwa. Sio nchi zote zina hayo mambo, yanakuja kwa jitihada. Sifa, heshima, hadhi na mafanikio ya nchi yana manufaa ya moja kwa moja kwa ustawi wa nchi, siyo kwa sifa ya kiongozi pekee bali kwa Mtanzania mmoja mmoja," alisema Waziri Makamba ambaye ni Mbunge wa Bumbuli.

Alisema hata uwapo kwa Watanzania nchini humo ni kutokana na sifa hizo kwa kuwa sera za Visa hutokana na sifa na heshima ya nchi hiyo, na kwamba jitihada za kujenga nchi ni za kuwarahisishia Watanzania ustawi wao na kwamba haviwezi kutenganishwa.

"Kuna dhana kwamba jitihada hizi za Rais Samia kukubali mialiko ya viongozi mbalimbali duniani kuja kuifanya kazi ya nchi yetu havina mahusiano ya moja kwa moja na maisha ya Mtanzania wa kawaida. Mahusiano ni makubwa sana tunategemea raslimali za misaada kutokana na mikopo ambayo hupatikana kutokana na haiba ya kiongozi mwenyewe," alisema na kuongeza:

Akizungumza katika hafla hiyo, Balozi wa Tanzania nchini Korea, Mavura Togolani, alisema ziara ya Rais Samia imewezesha nchi kupata fedha kwa ajili ya miradi ya miundombinu ambao umeongezeka hadi Dola bilioni 2.5, mazungumzo ya ushirikiano kwenye uchumi wa buluu na madini ya kimkakati ambayo yanafanya vizuri nchini humo.

Alisema mazungumzo yatakayowezesha kutia saini ushirikiano wa kiuchumi kati ya Korea na Tanzania kutokana na biashara kati ya Korea na Afrika ni asilimia moja, na biashara iliyopo na Tanzania ni dola 200 pekee na matarajio ni kuleta wawekezaji wengi kutokana na kuitambua kama nchi ya kushirikiana.

Awali, akisoma taarifa ya umoja wa Watanzania wanaoishi nchini Korea, Mwenyekiti wa Diaspora - Korea, Ally Hamad, alisema wana wanachama 250 na kati yao asilimia 60 ni wanafunzi pamoja na wafanyabaishara na wengine kwenye sekta binafsi, huku kukiwa na changamoto ya kukosa chanzo cha mapato cha uhakika cha kuendesha jumuiya hiyo.

Nyingine ni Diaspora kukosa njia nafuu ya kutuma fedha nyumbani ndio maana inaonekana mchango wao ni kidogo, huku wakitaka maboresho ya mifumo ili Watanzania wanaoishi nchini humo na kufanya akzi katika sekta mbalimbali wapate stahiki za mafao, kupandishwa vyeo na kuongezwa mshahara.

Aidha, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuingia mkataba na Korea ili Watanzania waweze kupata nafasi nyingi za ajira kwa kuwa nchi hiyo ina upungufu wa wafanyakazi 165,000, na kwamba kuna uwezekano wa kupata nafasi ya wengi kufanyakazi sehemu mbalimbali.

Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Mbeba mizigo akiwa na kiroba chenye matunda aina ya parachichi, kwa ajili ya kujipatia ujira wa siku katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama yabariki bodaboda anyongwe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Kanda ya Mtwara imebariki bodaboda Lucas Wage anyongwe hadi kufa kwa kumuua kwa kukusudia bodaboda mwenzake, David Dominick.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji Rehema Kerefu, Jaji Sam Rumanyika na Jaji Agnes Mgeyekwa baada ya kupitia hoja za rufani zilizowasilishwa na mrufani Lucas kupinga adhabu ya kunyongwa.

Lucas alitiwa hatiani na kupewa adhabu ya kunyongwa hadi kufa na Mahakama Kuu Mtwara baada ya kujiridhisha kwamba upande wa mashtaka umethibitisha kosa la kuua bila kuacha shaka.

Awali ilidaiwa kuwa Mei 22, 2019, katika Kijiji cha Mkalapa Bondeni, wilayani Masasi, Mtwara, mrufani alimuua kwa kukusudia Dominick.

Upande wa mashtaka katika shauri hilo ulikuwa na mashahidi wanane na katika ushahidi wao, shahidi wa pili alikuwa anamiliki bodaboda aina ya SanLG yenye namba za usajili MC 226BZJ.

Shahidi huyo alimpa mrufani bodaboda hiyo kwa makubaliano ya kupelekea hesabu ya Sh. 40,000 kila wiki, mrufani alishindwa kupeleka hesabu kama walivyokubaliana.

Inadaiwa mmiliki wa pikipiki hiyo alichukua mali yake na kumkabidhi Dominick (marehemu) kwa makubaliano ya kupeleka hesabu ya Sh. 40,000 kwa wiki. Shahidi anadai Dominick alikuwa anafanya vizuri, alipeleka hesabu kama walivyokubaliana.

Anadai kuwa Mei 22, 2019, saa nne usiku, shahidi alimpigia simu Dominick, lakini ilikuwa imezimwa, hivyo hakumpata. Alimtafuta siku iliyofuata bila mafanikio.

Shahidi anadai Mei 24, 2019, mume wake alimfahamisha kuwa Dominick amekutwa amefariki dunia na pikipiki yake imekutwa nyumbani kwa mrufani.

Shahidi wa tatu anadai katika ushahidi wake kwamba alimwona Dominick Mei 22, 2019 saa mbili usiku akiwa amesimama na mrufani.

Daktari katika ripoti ya uchunguzi iliyotolewa mahakamani, alibainisha kuwa kifo cha Dominick kilisababishwa na kukabwa koo.

Mrufani alijitetea kwa kudai alikuwa anamfahamu Dominick, walikuwa wanaishi kijiji kimoja, anamfahamu kuwa alikuwa anaendesha bodaboda, akakana kuhusika na tukio la mauaji.

Anadai hakushirikishwa katika upekuzi uliofanyika nyumbani kwake ambako pikipiki ilikutwa imefichwa chumbani.

Katika utetezi wake anadai ushahidi wa shahidi wa tatu ni stori ya uongo.

Mrufani aliwasilisha sababu za kupinga adhabu ya kunyongwa hadi kufa, akidai upande wa mashtaka haukuthibitisha kosa dhidi yake, hivyo mahakama ilikosea kisheria kumtia hatiani na kumpa adhabu hiyo.

Aliwakilishwa na Wakili Rainery Songea na Alex Msalenge huku upande wa Jamhuri ukiwakilishwa na Credo Rugaju na Faraja George. Jopo baada ya kupitia hoja za rufani na hukumu ya Mahakama Kuu, lilikubaliana na uamuzi wa jaji wa mahakama hiyo wa kumtia hatiani mrufani na kumpa adhabu ya kunyongwa hadi kufa.

"Kwa mazingira ya ushahidi ni kwamba mrufani ndiye aliyemuua David na kwa nyongeza mrufani alikuwa mtu wa mwisho kukutana na marehemu Mei 22, 2019 na alishindwa kutoa ufafanuzi kuhusiana na hilo.

"Kutokana na ushahidi wa shahidi wa kwanza hadi wanane ni kwamba mrufani kamuua David, bodaboda ilikutwa imefichwa nyumbani kwake, Mahakama Kuu ilikuwa sahihi, mashtaka dhidi ya mrufani yalithibitishwa bila kuacha shaka. "Mahakama inatupilia mbali rufani, haina mashiko, adhabu iliyotolewa na Mahakama Kuu ilikuwa sahihi," lilisema jopo.

# Waziri Mkuu ataka uwiano sawa walimu mijini, vijijini

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza maofisa elimu na wakurugenzi wa halmashauri zote nchini wafanye mapitio ya ikama zao kuangalia mrundikano wa walimu katika maeneo ya mijini na pembezoni mwa barabara na kuwasambaza katika maeneo ya vijijini ili kuwe na utoshelevu wa walimu katika maeneo yao.

Alielekeza hayo jana alipojibu swali la Mbunge wa Bahi, Keneth Nollo wakati wa kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu' bungeni jijini hapa.

Mbunge huyo alitaka kufahamu mkakati wa serikali kuruhusu majiji na halmashauri zenye uwezo ziajiri walimu na kuondoa tatizo la upungufu wa walimu nchini.

Waziri Mkuu alisema serikali imesimamia mifumo ya ajira na ajira zote za kudumu ziko chini ya Serikali Kuu, zikiwamo za sekta ya elimu.

Upungufu huo pamoja na mambo mengine, Majaliwa alisema unachangiwa na mpango usiokuwa mzuri wa kusambaza walimu kwenye baadhi ya halmashauri.

"Walimu wengi wanaonekana mijini kuliko vijijini. Lengo la kuwa na mfumo mmoja wa kuajiri na kupata kanzidata ya idadi ya waliopo kazini, wanaoajiriwa lakini pia kusambaza kwa usawa kwenye halmashauri zote ili kusiwe na halmashauri moja kuwa na mrundikano mkubwa kwa sababu tu wana uwezo wao kuajiri.

"Kwa hiyo, Serikali Kuu inasimamia kusambaza walimu kulingana na mahitaji," Waziri Mkuu Majaliwa alisema.

Kiongozi huyo pia alisema Tanzania ina sheria za kazi ambazo zinaainisha muda wa kuingia na kutoka kazini na kwa mujibu wa sheria hizo, muda wa kazi kiserikali ni saa nane kwa siku za kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi 9.30 alasiri.

Aliyasema wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mariam Kisangi aliyetaka kufahamu mpango wa serikali kupitia upya utaratibu wa watumishi wa kada moja kutoka kazini. Alisema walimu wa mijini na vijijini wamekuwa wakitofautiana muda wa kutoka kazini.

Waziri Mkuu alisema utofauti wa muda wa kutoka kwa walimu wa vijijini na mijini ni mazingira ya maeneo hayo kwa kuwa maeneo ya mijini wanafunzi na walimu wakiingia asubuhi, mchana hawapati muda wa kupumzika, hivyo huunganisha hadi saa 9.30 na vijijini hupata muda wa nafasi ya kwenda kula na kurudi tena na muda huo ndio unaofidiwa, saa za kazi ni zilezile.

"Huu ni mpangokazi uliowekwa kulingana na mazingira yaliyopo, kwanini mjini wanaamua kuunganisha moja kwa moja?

"Kwanza, kuna shida ya usafiri, huwezi kumruhusu mchana arudi nyumbani na aende tena shuleni, ni shida lakini vijijini kwa kuwa hakuna tatizo la usafiri wanatembea kwenda na kurudi," Majaliwa alifafanua.

# Mkumbo: Wawekezaji kutoka Korea watafurika

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, amesema Tanzania imekopa Dola za Marekani bilioni 2.5 kutoka Korea, sio kwa lengo la kulipa mishahara ya umma, bali kwa nia ya kujenga misingi ya kisekta.

Alisema baada ya Tanzania kutia saini mkataba wa makubaliano na Korea, kuiwezesha nchi kupokea mkopo kwa kipindi cha mwaka 2024 hadi 2028, sasa wawekezaji kutoka nchi hiyo 'watafurika' nchini.

Profesa Kitila, aliyasema hayo jana, Ikulu, jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano ulioandaliwa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ukihusisha viongozi wa serikali na waandishi wa habari, ikiwa ni mrejesho wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, nchini Korea.

Alisema kwamba kwa miaka 20 mfululizo nchini, uwekezaji wa ndani unawahusisha wawekezaji kutoka bara la Asia, ikilinganishwa awali wengi walitoka bara la Ulaya na Amerika.

"Sasa tunauza wapi, tunauza zaidi Asia. Kikubwa tunachokitarajia ni kuongeza wawekezaji kutoka Korea. Mkopo huu sio wa kwanza na hakuna mkopo hata mmoja ambao uliweka rehani rasilimali za asili.

"Kukopa muhimu, kwanza kujenga mtaji, unakopa wapi na masharti gani? Tumejiwekea utaratibu ni kutumia uwezo wa ndani, kuchukua mikopo ambayo sio ya kibiashara yenye masharti nafuu, hatujakopa kulipana mishahara ni kujenga uwezo kisekta.

"Tutalipa kwa miaka 40 na tutalipa kwa riba ya 0.01 kimsingi unaanza kulipa lipi?... Tunakwenda kujenga uwezo wa uzalishaji, elimu, afya, chuo cha TEHAMA," alisema Prof. Kitila.

Tanzania imeshiriki Mkutano wa Wakuu wa Serikali kati ya Korea na Afrika katika mji wa Goyang, Seoul Korea, ukiwaleta pamoja marais 25 na wawakilishi wa wengine 23 barani humo, kujadili ushirikiano baina ya nchi hiyo na ukanda huo.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema bidhaa 10,998 zimeruhusiwa kupelekwa Korea bila ushuru, na kati ya hizo 1,126 zinazotoka katika sekta ya kilimo huku zikipelekwa pamba na tumabaku.

Alisema Tanzania inafanya biashara kwa asilimia moja pekee na Korea, kutokana na viwango duni vya bidhaa, na kwamba makubaliano hayo yanahusisha pia elimu ya namna ya kuzalisha bidhaa za viwango na kukubalika katika soko la dunia.

"Bidhaa yetu inakosa kanuni ya uasili, kwamba bidhaa hii inatoka wapi? Tupaswa kuongeza thamani na kufikia asilimia 80 na kuwapo uendelevu wa bidhaa zetu sokoni."

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya, alisema kisiwani humo kutakuwa na huduma za afya kimataifa, baada ya kupata mkopo kutoka Korea na kuwekeza kwenye sekta hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema ushirikiano wa kimataifa kwenye maendeleo na ushirikiano wa kuvutia masoko na maarifa kunahitajika nchi nyingi ili kupanua wigo wa biashara kwa bidhaa za Tanzania.



Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Epson Luhwago, akikata keki kusherehekea miaka 55 ya kuzaliwa, wakati wa hafla fupi iliyofanyika katika chumba cha habari cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni wafanyakazi wenzake. **PICHA: JOHN BADI**

# Marekani yaimarisha mapambano dhidi malaria mikoa kusini Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani imeongeza juhudi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria nchini Tanzania kwa kukabidhi zana muhimu za kusaidia watoa huduma wa matibabu ya afya katika ngazi ya jamii kusini mwa Tanzania ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Lindi.

Kupitia mradi unaofadhiliwa na Mpango wa Rais wa Marekani wa Kudhibiti Malaria (PMI), unaoitwa Dhibiti Malaria unaotekelezwa kwa ushirikiano wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) na Kituo cha Kuzuia Magonjwa cha Marekani (CDC), Serikali ya Marekani imetoa vifaa vya thamani ya Sh. milioni 47.5 ikiwamo baiskeli, simu janja, mizani, vipimajoto na zana nyingine kwa watoa huduma 75 wa usimamizi wa huduma za matibabu ngazi ya jamii (iCCM) kutoka halmashauri tisa za mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani.

Taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani jana, ilisema watoa huduma hao wamepatikana kwa kupitia ushirikishwaji wa viongozi kutoka jamii zao na kupata mafunzo kwa msaada unaotolewa kwa ushirikiano na Mpango wa Rais wa Marekani wa Kudhibiti Malaria (PMI), watoa huduma hao wapya wanaosimamia huduma za matibabu ngazi ya jamii waliopata mafunzo sasa wana vifaa wanavyohitaji ili kutambua na kutibu malaria, nimonia na kuhara kwa watoto katika baadhi ya maeneo ya kusini mwa Tanzania ambazo zinahitaji sana hiyo huduma na ambazo ni ngumu kufikika.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Zuwena Omary, aliishukuru Serikali ya Marekani kwa kupunguza adha ya ugonjwa wa malaria mkoani humo na kuipongeza Serikali ya Tanzania kwa ukarimu wa watu wa Marekani na kuendelea kusaidia mashirika yanayotekeleza programu za malaria nchini Tanzania.

"Tunaamini watoa huduma za matibabu ngazi ya jamii hawa wapya watasaidia pia kuimarisha huduma za ngazi ya kituo na kuchangia katika kupunguza malaria, na kufikia malengo ya muda mrefu ya kutokomeza malaria," alisema Mtaalamu wa Mradi kutoka USAID, Albert Ikonje akizungumza katika hafla ya makabidhiano hayo.

Tangu mwaka 2006, Serikali ya Marekani imechangia zaidi ya dola milioni 747 kukabiliana na ugonjwa wa malaria nchini, ikijumuisha msaada wake na juhudi za kimkakati za kitaifa za Serikali ya Tanzania.

Msaada huo umechangia kupungua kwa maambukizi ya malaria kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia nane mwaka 2022, kulingana na Utafiti wa Demografia wa Afya/Viashiria vya Malaria Tanzania wa 2022.

PMI Dhibiti Malaria, ni mradi wa dola milioni 27, unaotekelezwa na Population Services International Tanzania, uliaonza mwaka 2022 - 2027.

# Bunge laazimia halmashauri kununua magari na vifaa zimamoto na uokoaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na upungufu wa magari ya zimamoto na vifaa vinavyotumika kuzima moto na uokoaji, Bunge limeazimia mambo matano, ikiwamo kupelekwa bungeni Muswada wa Sheria ili kuweka utaratibu wa kuwezesha halmashauri kutenga fedha katika bajeti zao.

Fedha hizo ni kwa ajili ya kununua magari ya zimamoto, vifaa na matengenezo ya magari na vifaa vya zimamoto na uokoaji.

Azimio lingine ni serikali kupeleka bungeni muswada wa sheria utakaoweka utaratibu wa kuwezesha halmashauri za miji na wilaya kuingia makubaliano ya ushirikiano (MoU) na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kununua magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji.

Pia serikali ipeleke bungeni muswada wa sheria utakaoweka utaratibu wa utekelezaji wa Sera ya Huduma kwa Jamii (CSR) kuwezesha miradi mikubwa ya kimkakati kuweka huduma za zimamoto na uokoaji.

Pia imeazimiwa serikali kupeleka bungeni muswada wa sheria utakaoweka utaratibu wa kuwezesha uwekaji wa 'Fire Hydrants' katika miradi yote ya maji na kuingia makubaliano ya ushirikiano kati ya mamlaka za maji nchini na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika uwekaji na ukarabati wa vifaa hivyo.

Kadhalika, imeazimiwa serikali kuweka utaratibu maalum wa kuwezesha upatikanaji wa ajira kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuajiri askari wengi kila mwaka ili kukidhi shughuli za uokoaji na kupambana na majanga nchini.

Maazimio hayo yamefikiwa baada ya Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (CCM) kuwasilisha hoja binafsi kuhusu halmashauri za miji na wilaya kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika kutatua tatizo la upungufu wa magari ya zimamoto pamoja vifaa vinavyotumika kuzima moto na uokoaji.

Akiwasilisha hoja yake, alisema licha ya halmashauri kuruhusiwa kutumia fedha kutoka vyanzo vilivyopo kwenye eneo husika katika kutekeleza miradi iliyopo kwenye maeneo yao, bado yako baadhi ya masuala ambayo halmashauri hazina mamlaka ya moja kwa moja katika kupanga na kutenga bajeti ya mambo inayoona ni muhimu kuitekeleza.

Alisema moja ya masuala hayo ni halmashauri za miji na wilaya kushindwa kuyatekeleza katika muda ambao halmashauri inaona inafaa ni ununuzi wa magari ya zimamoto na vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kuzima moto na uokoaji.

Ugumu huo, alisema unatokana na halmashauri kushindwa kutumia fedha zake kutekeleza miradi husika kutokana na misingi ya kisheria.

"Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 2007, masuala yote ya huduma ya zimamoto na uokoaji yalikuwa yanasimamiwa kwa ukaribu na Serikali za Mitaa kupitia halmashauri za miji na wilaya," alisema.

Alisema halmashauri hizo zilihusika kikamilifu katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za zimamoto na uokoaji kwa kutenga bajeti kuhusu masuala yanayohusu ununuzi wa magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji.

"Mheshimiwa Spika, kutokana na kutungwa kwa Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mwaka 2007, tangu wakati huo hadi sasa masuala yanayohusu ununuzi wa magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji yanafanyika na serikali kuu kupitia jeshi hilo.

"Aidha, tangu jukumu hilo kuhamishiwa katika jeshi hilo, kumeendelea kuwapo ukosefu na upungufu mkubwa wa magari na vifaa vya zimamoto na uokoaji katika halmashauri nyingi kwa kuwa serikali kuu inakosa fedha za mkupuo kununua magari kwa halmashauri zote chini," alisema.

Alisema jambo hilo limesababisha wabunge wengi kuiuliza serikali mara kwa mara maswali kuhusu kutokuwapo kwa magari ya zimamoto, ubovu wa magari ya zimamoto, umbali mrefu kutoka magari ya zimamoto yalipo hadi mahali ambapo majanga yanatokea na kutokuwapo kwa vifaa toshelezi na vya kiasasa vya zimamoto na uokoaji.

Kadhalika, alisema matarajio ya wabunge wote ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya zimamoto na uokoaji kwa haraka na kwa ufanisi.

"Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005 ibara ya 147 (1) na (2) na ibara ya 148 (1) inaeleza madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu kuunda jeshi la aina yoyote na kuyaamuru majeshi hayo katika kuokoa maisha na mali za watu katika hali ya hatari na hapo ndipo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipoundwa kwa lengo kuu la kuokoa maisha na mali.

"Aidha, sina shaka na uhodari na uwezo wa askari wa jeshi hili bali wanahitaji vifaa vya uokoaji na magari ya kuzima moto ya kutosha katika kutimiza majukumu yao kisheria na kikatiba katika kuhakikisha usalama wa wananchi," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali kuu ibakie na jukumu la kutoa maofisa na askari hodari na wazalendo lakini halmashauri zipewe jukumu la uwekaji wa miundombinu wezeshi ikiwemo magari ya kuzima moto na vifaa katika shughuli za uokoaji nchini.

Alisema, serikali imekuwa na miradi mikubwa ya kimkakati kama vile Standard Gauge Railway (SGR), Julius Nyerere Hydroelectric Power, Bomba la mafuta la Uganda na Tanzania, miradi hi mikubwa inategemea huduma ya zimamoto na uokoaji kutoka katika vituo vya zimamoto na uokoaji vilivyo mijini ambapo ni mbali na eneo ilipo.

Alisema miradi hiyo inahitaji huduma ya zimamoto na uokoaji kwani inaweza kupata hitilafu na kutokea ajali ya moto na majanga mengine na pengine kukwamisha mradi kuendelea.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matumizi mabaya ya fedha yapigwe vita kila mahali

**KATIKA** mataifa mbalimbali hasa yaliyoendelea, moja ya mambo ambayo yamekuwa yakiheshimu ni utunzaji wa sarafu zao hasa noti ndiyo maana zimekuwa zikidumu kwa muda mrefu. Kutokana na kuheshimu sarafu zao, mtu anapotaka kufanya mwamala wowote akiwa na fedha ya nje ya nchi husika, hukataliwa au akikubaliwa atarudishiwa chenji yenye thamani ya kile anachorejeshewa.

Wakati mwingine, mtu anapokwenda kununua bidhaa na akawa na noti iliyochoka au kuchakaa, hukataliwa. Yote hiyo ni kuheshimu fedha hizo ambayo ni moja ya tunu za nchi. Pia mtu akiiharibu noti katika nchi hiyo ni anachukuliwa adhabu kali ikiwamo kufungwa jela.

Nchi kama Marekani inayotumia Dola, Uingereza (Pauni) na nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya ambazo zinatumia Euro, zimekuwa zikiheshimu sana fedha zao ndiyo maana hazichakai. Hata baadhi ya nchi za Afrika kama Msumbiji, Afrika Kusini na Botswana, kutokana na kuheshimu sarafu zao, ni nadra kukutana na noti zilizochakaa. Hata utunzaji wake ni mzuri ndiyo maana zinadumu.

Aidha, kutokana na utunzaji na kuheshimu fedha zao, mataifa hayo pia kiuchumi yako imara na sarafu zao ziko juu kulinganisha na mataifa yale ambayo noti zao hazitunzwi ipasavyo na kuharibika haraka.

Tanzania, kwa mfano, wananchi wengi hawana utamaduni wa kutunza fedha hizo ili zidumu kwa muda mrefu ndiyo maana niyo ikitoka benki na kuingia kwenye mzunguko baada ya muda mfupi huchakaa na kupoteza ubora wake.

Sababu kubwa ni kwamba hupita katika mikono mingi ya watu ambao wengine hujihusisha na biashara kama ya mkaa, mafuta na kukaanga samaki. Pia watu wengi huzikunjakunja fedha hizo badala ya kuziweka vizuri katika pochi, hivyo kusababisha noti kupoteza ubora na thamani.

Hata utunzaji wa fedha hizo si sahihi kwa kuwa baadhi ya watu wamekuwa wakiweka kwenye matiti, nguo za ndani, soksi, chini ya magunia, vibuyu, kufunga mafundo kwenye kanga, au kwenye mifuko ya plastiki na kuziweka chini ya sakafu au kuzichimbia chini.

Mbali na utunzaji huo ikiwamo kuweka fedha sehemu za siri, umezuka mtindo wa watu kwenye sherehe kama harusi na kipaimara, kutengeneza mataji kwa kutumia noti hasa za Sh. 10,000 na kuwatunza wahusika.

Kutokana na utunzaji huo usio mzuri na matumizi mabaya ya fedha, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeonya watu kwa kile ilichosema kwamba ni kuidhalilisha sarafu ya nchi na kuonya kuwa watakaobainika kufanya hivyo, watachukuliwa hatua za kisheria, ikiwamo kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria, kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Kwa ujumla, noti au sarafu ya nchi, kwa maana ya Shilingi kwa Tanzania, ni moja ya tunu za taifa, hivyo zinapaswa kuheshimiwa na kuthaminiwa na kila mtu. Kwa mantiki hiyo, kutozitunza ipasavyo na kuzitumia kinyume na makusudi, ni ufedheheshaji wa tunu hiyo adhimu kwa taifa.

Haya nyakati fulani, baadhi ya viongozi wa ngazi za juu serikalini, wakiwamo mawaziri, wamekuwa wakizitaja fedha za Tanzania kwa dharau kwa kuziita fedhe za madafu. Kutokana na umuhimu wa sarafu ya nchi na kwa kuwa ni utambulisho wa taifa, kuziita fedha kwa majina ya dharau ni udhalilishaji.


Ni wakati mwafaka sasa jitihada zikafanyika kuelimisha umma kuhusu utunzaji mzuri wa fedha ya Tanzania ili idumu kwa muda mrefu na kwa maendeleo ya uchumi wa taifa. Msisitizo mkubwa wa elimu uwe kuanzisha shule za msingi ili kujenga kizazi kijacho chenye nidhamu na heshima kwa sarafu ya nchi.


Kwa kuwa suala hili ni mtambuka, viongozi wa serikali, madhehebu ya dini, asasi za kiraia na mwananchi mmoja mmoja kuelimisha watu juu ya matumizi sahihi ya noti. Pia kwa wale wanaoshiriki katika miamala mbalimbali, wanapopewa noti iliyochakaa, wakatae ili kuwafanya watu kuwa na nidhamu katika utunzaji wa fedha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi wasiache kutenga bajeti ya taulo za kike kwa mabinti zao

**KILA** mzazi wenye mtoto wa kike ambaye kapevuka, ana wajibu wa kumtengea bajeti ya taulo ngumu kila mwezi, ili kumsaidia katika usalama wa maisha hayo.

Hedhi salama inamsaidia mtoto kuwa huru na kama ni mwanafunzi, anapofika hatua hiyo anaishi pasipo shaka yoyote, juu ya usalama wake.

Kwa baadhi ya familia, suala la hedhi salama kwa mtoto wa kike, wanaona suala hilo linasimamiwa na mzazi mmoja ambaye ñi mama na sio baba. Kiuhalisia, suala la hedhi salama linatakiwa kuzingatiwa na wazazi wote katika kumtengea mtoto bajeti yake kila mwezi.

Ni lazima lizingatiwe ili kumwezesha mtoto wa kike kuyafikia malengo yake.

Wapo wanafunzi wa kike wanashindwa kuyafikia malengo yao kutoka na kukosa vifaa vya kujistiri wakati wa hedhi.

Wapo wanakuwa na vifaa vya kujistiri, lakini changamoto nyingine inakuja pale mwanafunzi anapokosa chumba cha kujisitiri.

Hayo yote yakifanyiwa kazi, maana yake, yatamsaidia mtoto wa kike kuwa katika hedhi salama kila mwezi. Hivyo, wazazi na walezi nchini wanatatakiwa kuhakikisha wanawawezesha watoto wa kike kila mwezi kupata vifaa vyao vya kujilinda na kuwa na hedhi salama katika muda husika.

Ni sauti inayotolewa na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Molel, katika kilele cha maadhimisho ya jumla ya Hedhi Salama Duniani, kitaifa yakiidhimishwa jijini Arusha.

"Wazazi mara nyingi tumekuwa tukitenga bajeti ya kununua vitu mbalimbali kwa ajili ya matumizi majumbani kwetu.

"Lakini, eneo hili la kununua pedi 'taulo za kike' mara nyingi tunakuwa tunalisahau, niwaombe wazazi na walezi wote tutenge bajeti ya kila mwezi kwa ajili ya kuwezesha hawa mabinti zetu waweze kuwa na uhakika wa kuwa na taulo za kike na kufikia malengo ya hedhi salama," anasema.

Anaongeza kuwa, serikali imekuwa ikihimiza uwekezaji wa uzalishaji bidhaa za hedhi nchini ili ziweze kupatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Pia, katika hilo anapongeza mchango wa wadau wa sekta tajwa, katika kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa taulo hizo.

"Napenda kutoa pongezi kwa Kiwanda cha A-Z kilichopo hapa Arusha, kwa kuanzisha uzalishaji wa bidhaa hizi muhimu nchini, ambayo kwa sasa wanazalisha taulo za kike zitakazoweza kutumika kwa muda mrefu," anasema.

Anafafanua kuwa, pia wanakaribisha wazalishaji wengine kujitokeza kuwekeza kwenye uzalishaji wa bidhaa za hedhi, ili ziweze kupatikana kwa wingi na kwa gharama nafuu nchini.

Akisoma taarifa ya Jukwaa la Hedhi Salama nchini, Mariam Mashimba, Mwenyekiti wa jukwaa hilo anasema hivi sasa watumiaji wengi katika shule wanapendelea taulo za kufua.

"Wakati wa utafiti asilimia 75 ya wanafunzi waliohojiwa katika baadhi ya shule za sekondari na msingi ndani ya mikoa 22, ambako utafiti ulifanyika, walionyesha kupendelea zaidi taulo za kufua kwani huokoa uchumi wa wazazi wao na kutunza mazingira, pia huondokana na adha ya kukosa mahali pa kutupa pindi wanapomaliza kutumia," anasema.

Mwakilishi wa Mkoa wa Arusha, Dk. Omary Chande, akitoa salamu za mkoa, anasema mkoa wa Arusha ni miongoni mwa mikoa iliyopokea fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza afua za afya.

"Katika mwaka wa fedha 2023/24 mkoa ulipokea zaidi ya Sh. bilioni 33.2 za uboreshaji wa miundombinu ikiwapo Hospitali ya Mkoa, wilaya na vituo vya afya," anasema.

HABARI KITAIFA

# 'Ipo haja kuwapo sera ya maendeleo zao la mwani'

**Na Jenifer Gilla**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, amesema kuna haja ya kutengeneza sera inayoongoza utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya zao la mwani ili lilete mafanikio kwa wakulima na kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

Kauli hiyo ilikuja baada ya wakulima wa zao hilo kulalamikia changamoto ya uhaba wa soko na madalali kupanga bei ya ununuzi jambo linalowarudisha nyuma.

Shemdoe aliyasema hayo juzi katika kikao kilichojadili mwenendo wa biashara ya mwani nchini kwenye mkutano wa hali ya uvuvi barani Afrika ulioratibiwa na Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira (WWF) Tanzania jijini Dar es Salaam.

Alisema mwaka 2005 serikali iliandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya mwani ambao utekelezaji wake haukufanyika kutokana na kutokuwapo na sera ya kuwaongoza na kwamba ni wakati sasa wa kutengeneza sera ili iwe rahisi kutekeleza mikakati iliyopo.

Alisema sera hiyo pia itasaidia kutoa mwongozo kwa jumuiya au vyama vitakavyoundwa ili kusaidia wakulima kunufaika sawa sawa na nguvu wanayoitumia kuzalisha zao hilo.

Alisema wizara imejizatiti kuweka mazingira rafiki kwa wakulima wa zao hilo nchini kwa kushughulikia changamoto zao ikiwamo kuhakikisha wakulima wanauza zao hilo kwa bei rafiki kwao na wanunuzi.

Kiongozi wa Programu ya Bahari WWF, Dk. Modesta Medard, alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo wakulima wa mwani ni bei na kutaka serikali ifanye utaratibu wa kuwabana madali ili wasiweke bei zinazowaumiza wakulima kwa sababu wanatumia nguvu kubwa kuzalisha.

Akisoma taarifa ya hali ya mwani nchini Mwenyekiti wa Kongano la Mwani, Zanzibar (ZaSCI) Dk. Flower Msuya, alisema licha Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa zao hilo Afrika bado inapitia changamoto ya uhaba wa masoko, madalali wanaowanyonya wakulima na uhaba wa vifaa vya kisasa vya kuchakata zao hilo.

Alisema kuna haja kuboresha teknolojia ili wakulima wawe na uwezo wa kuzalisha katika maji mafupi na marefu na kukauka bila kuathiri ubora wake.

Mkulima wa mwani kutoka Pemba, Fatma Machalila, alisema wanapata faida ndogo ikilinganishwa na nguvu wanayowekeza kwa sababu madalali wanaonunua kutoka kwao wanajipangia bei hali inayowarudisha nyuma na kuwakatisha tamaa ya kuendelea na uzalishaji.

Aliiomba serikali kuwatafutia masoko watayokuwa wanauza moja kwa moja ili kuepuka unyonyaji wanaofanyiwa na madalali hao.

Aliishauri pia serikali kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu faida ya mwani kwa Watanzania ili waone umuhimu wa kununua na soko la ndani liwe kubwa kama ilivyo kwenye mazao kama samaki.

Naye Machano Ally, aliiomba serikali kuwatafutia wateja watakaonunua mwani ukiwa bado mbichi ili kuwapunguzia wakulima gharama za kukausha kwa kuwa zinawaongezea hasara, pia hushusha kiwango cha zao hilo kutokana na vifaa hafifu vya kukaushia.



Wafanyakazi wa Barrick Bulyanhulu wakishiriki kufanya usafi katika maeneo yanayozunguka Kituo cha Afya cha Bugarama, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga juzi, katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Afrika yasisitizwa mikakati kuendeleza wavuvi wadogo

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, ametoa rai kwa serikali za Afrika kufanya kazi kwa kutengeneza mifumo mizuri pamoja na kuwapatia elimu wavuvi, kuwatengenezea mazingira ya kupata mitaji na masoko kwa ajili ya kuuza bidhaa zao za uvuvi.

Pia alisema kuwa Tanzania ina fursa kubwa ya kuendeleza viumbe maji kutokana na wingi wa rasilimaji maji kama bahari, maziwa, mito na mabwawa na makadirio ya uzalishaji wa samaki wa kufuga imefika tani 45,415 ambayo ni sawa na asilimia tisa.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika mkutano wa kilele wa wavuvi wadogo barani Afrika 2024, uliokutanisha pamoja wadau wa uvuvi kutoka mataifa 32 kwa lengo la kubadilishana uzoefu na namna ya kuendeleza uvuvi mdogo Afrika, alisema serikali imefanya jitihada za kuendeleza sekta hiyo kwa kuandaa na kutekeleza sera, sheria, kanuni na miongozo ya kuongeza miundombinu ya masoko.

Alisema serikali itaendeleza kukaribisha viwanda vya uchakataji, sehemu za kuhifadhia, na kugawa boti za kisasa, vizimba vya samaki pamoja na kutoa pembejeo za ufugaji wa samaki chakula na vifaranga na kutoa misamaha ya kodi kwa waingizaji wa vifaa vya uzalishaji wa samaki.

Aidha, alisema ziko changamoto zinazotakiwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka ikiwamo athari za maafa na mabadiliko ya tabia ya nchi, ushirikishwaji mdogo wa wadau katika usimamizi wa shughuli za uvuvi hususani wanawake na vijana.

"Maamuzi mtakayotoka nayo katika mkutano huu yatapaza sauti ya pamoja itakayowasilishwa na kamati ya kitaifa ya uvuvi katika mkutano wa kimataifa wa wavuvi wadogo utakaofanyika Italia, nitoe wito kwa jumuiya za kimataifa nazo kuweka sauti ya pamoja za kuwapigania na kuwasemea wavuvi," alisema Dk. Biteko.

Waziri wa Mifugo na Uvuzi, Abdallah Ulega, alisema ni heshima kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo wa kwanza kufanyika Afrika, ambao lengo lake kuu ni kutoa fursa ya kushiriki na kupaza sauti katika kuwezesha ushirikishwaji, uboreshaji wa sheria na kanuni zote zinazohusu wavuvi wadogo.

Alisema mkutano huo pia ni kwaajili ya kusherehekea miaka 10 ya utekelezaji wa mwongozo wa hiari wa uvuvi mdogo ili kufikia uvuvi endelevu na kwamba utafanya tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa mwongozo huo na muundo wa kisera, mikakati na ukuzaji viumbe hai Afrika.

"Mkutano huu umewaleta pamoja washiriki zaidi ya 470 na tunatumaini maazimio tutakayofikia yatasaidia katika kuboresha sekta ya uvuvi na mnyororo wa thamani wa zao la uvuvi katika nchi za Afrika," alisema Ulega.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk. Tito Nyabenyi, alisema wanawake wanachangia zaidi ya asilimia 20 katika pato la uvuvi Afrika na kuwa wavuvi wadogo ni uti wa mgongo wa sekta hii na familia zao zinawategemea katika suala la chakula na uchumi licha ya kukutana na changamoto mbalimbali.

Alisema jukwaa hilo linatoa fursa kwa wadau kushiriki mawazo mbalimbali, akibainisha kuwa changamoto kubwa wanazokutanazo ni mabadiliko ya tabianchi na kwamba wataendelea kufanya majadiliano na wadau wengine katika kuona namna bora ya kukuza na kuendeleza sekta hiyo.

"Tusikilize sauti za wavuvi, na mkutano huu utakuwa ni taswira ya kudumu, katika kushughulikia matatizo ya wavuvi, na ninampongeza Waziri wa Uvuvi Abdallah Ulega kwa kushiriki katika kufanikisha hili," alisema Tito.


Angela Matumba, mwakilisi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (SADC), alisema mkakati wa uvuvi una nafasi kubwa katika uchumi wa buluu hasa katika suala la chakula na kwamba watahakikisha wanaweka vipaumbele kwa ajili ya kuendeleza wavuvi wadogo.

"Inafurahisha kuona Tanzania imeonyesha kuwajali wavuvi wadogo, na uvunaji mkubwa wa samaki unatoka hapa, utafiti wetu ulibaini kwamba ni karibu asilimia 88 wanajihusisha na uvuvi. Na kuna uhitaji wa kuongeza msaada kwa wanawake katika kuendeleza sekta hii.

Hellen Gubama, Mwakilishi kutoka Umoja wa Afrika (AU), alisema umoja huo unapendekeza kusimamiwa zaidi haki za wavuvi wadogo wakiwemo wanawake pamoja na kuwaendeleza. Huku akiipongeza serikali ya Norway kwa kuendelea kuunga mkono Afrika kuendeleza sekta ya uvuvi.

Dk. Michael Bizwick mwakilishi kutoka nchini Malawi, alisema changamoto wanazokutana nazo wavuvi wa Tanzania ni sawa na wanazokutana nazo Malawi, ikiwemo suala la soko, na kwamba licha ya matatizo hayo, wanatakiwa kujadili na kuleta matokeo chanya yatakayowagusa wavuvi wote katika sekta hiyo.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# NFRA kununua mahindi ya wakulima Julai 15

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo imesema itaanza kununua mahindi ya wakulima nchini kati ya Julai 15 na 20, mwaka huu kupitia vituo mbalimbali vitakavyotangazwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alibainisha hayo jana jijini hapa, wakati wa hafla ya utiaji saini randama za ushirikiano kati ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

"Bora tusimamishe kila kitu, lakini sio kuacha mahindi yaharibikie mikononi mwa wakulima, hivi sasa NFRA, inaandaa mikataba ya wakulima na baadaye itatangaza vituo pamoja na bei hivyo wakulima watulie tutanunua mahindi yao yote na kwa bei nzuri wasisumbuliwe na madalali," alisema Bashe.

Akizungumzia tukio la utiaji saini na ushirikiano huo, Bashe alisema wizara yake imekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na WFP ikiwamo kuiuzia mahindi meupe, maharagwe pamoja na mtama.

"Makubaliano ambayo tumeingia leo na WFP itaweza kununua mahindi tani 60,000 zitazogharimu Dola za Marekani milioni 22, lakini pia tutanufaika na ushirikiano huu kwa watendaji wetu wa CPB na NFRA kujengewa uwezo ili kuongeza ubora kwenye kuhifadhi mahindi yetu na biashara kwa ujumla," alisema Bashe.

Awali, Mkurugenzi Mkazi wa WFP, Sarah Gordon-Gibson, alisema wana ushirikiano wa muda mrefu kati yao na NFRA pamoja na CPB kuhakikisha usalama wa chakula na lishe nchini kupitia afua kadhaa.

"Kuanzia 2011 hadi 2023, WFP imenunua kutoka NFRA zaidi ya tani 223,000 za mahindi meupe na karibu tani 4,000 za mtama kwa thamani ya jumla ya zaidi ya dola milioni 60 za Marekani," alisema.

Aidha, alisema mwaka huu WFP, inapanga kununua tani 60,000 za mahindi meupe kutoka NFRA na CPB kwa thamani ya Dola za Marekani milioni 22.

WFP, imekuwa ikikodisha maghala ya NFRA mjini Dodoma kuanzia mwaka 2011 hadi 2023 kwa Dola za Marekani 213,000.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa NFRA, Dk. Andrew Komba, alisema mahusiano yao na WFP ni zaidi ya miaka 10 licha ya kufanya biashara ya mahindi pia Shirika hilo limesaidia kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

"Katika makubaliano haya ya leo licha ya kuuza mahindi meupe tani 60,000 zitakazogharimu kiasi cha Dola za Marekani miloni 22, pia tutanufaika na 'staff' wetu kujengewa uwezo katika masuala mbalimbali ikiwamo biashara pamoja na uwezo wa kifedha," alisema Dk. Komba.



Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), Godson Mollel (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu tamko la chama hicho la kulaani tukio la kutekwa mtoto mwenye ualbino mkoani Kagera na kutaka uchunguzi wa tukio hilo uharakishwe. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa TAS Mkoa wa Dar es Salaam, Gabriel Aruga. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bosi adaiwa kumchoma moto mfanyakazi wake wa ndani

**Na Rose Jacob,**
MWANZA

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamshikilia Christina Shiriri, maarufu Manka (43), mfanyabiashara mkazi wa Usagara, wilayani Misungwi, mkoani hapa kwa tuhuma za kummwagia mafuta ya taa mfanyakazi wake wa ndani na kumchoma moto.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Wilboard Mutafungwa, alisema binti aliyefanyiwa ukatili huo ni Grace Joseph (17), mkazi wa kijiji cha Nyalwigo wilayani Misungwi kwa kudaiwa kumwibia fedha bosi wake Sh. 161,000.

"Tukio hilo, lilitokea Juni 4, mwaka huu, majira ya 2:00 ambapo Christina, alidai kuibiwa fedha zake kiasi tajwa hapo juu alizokuwa amezihifadhi chumbani kwake, alipomuuliza Grace kuhusu hela hizo, alikiri kuzichukua na alizirudisha kwa mwanamke huyo, baada ya kuzirejesha, ndipo bosi huyo aliamua kumtendea ukatili huo kwa kummwagia mafuta na kumchoma mwilini mzima," alisema Mutafungwa.

Alisema Grace, amepelekwa Hospitali ya Wilaya ya Misungwi, kwa ajili ya matibabu na mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa, atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Aidha, Mutafungwa, alitoa rai kwa wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi, wakati wanapo watuhumu watu wanaofanya makosa na badala yake wawafikishe katika vyombo vya sheria, kwa ajili ya hatua stahiki na waendelee kutoa taarifa za wahalifu kwa Jeshi la Polisi.

# Wanafunzi wakalia viroba kwa kukosa madawati

**Na Beatrice Moses**

UHABA wa madawati unatajwa kuzikabili shule kadhaa Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam ikiwamo Shule ya Msingi ya Saranga ambayo baadhi ya wanafunzi wanalazimika kubeba viroba (mfuko wa salfeti) kukalia darasani.

Shule hiyo ipo katika Mtaa wa Ukombozi, Kata ya Saranga, inayohudumia wanafunzi kutoka katika mitaa minne ya Golani, Ukombozi, Saranga na Upendo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Saranga, Braxton Mwakilanga, amekiri kuwapo kwa tatizo la upungufu wa madawati na madarasa.

Shule hiyo ina wanafunzi 2,400 vyumba vya madarasa 19 kati ya hivyo vitatu ni vipya ambavyo havijakamilika kwa kutumika, wakati mahitaji ni 57, madawati yaliyopo ni 300 upungufu ni 450.

"Nimeshiriki kikamilifu kusaka wadau wa kutusaidia kutatua changamoto hii, wengine wamejibu wengine hawajajibu, hivi karibuni tulipokea madawati 100 tunashukuru, bado tuna uhitaji mkubwa wadau watusaidie watoto wasome kwa utulivu unaostahili," alisema Mwakilanga aliyedumu kwenye nafasi hiyo tangu 2017.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Aron Kagurumjuli, ambaye kwa mujibu wa utaratibu wa shule za serikali ndiye msemaji, aliruhusu Ofisa Elimu wa Shule za Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo, Denis Nyoni, kuzungumzia hali ilivyo.

Nyoni alisema, serikali inafanya juhudi kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, lakini nguvu za wadau zinahitajika ili kupata suluhisho haraka.

**HALI ILIVYO**

Tangu Januari 29, mwaka huu, mahitaji ni madawati 35,496, yaliyopo ni 22,409.

Alisema Sh. milioni 700 zimetengwa kwa ajili ya kutengeneza madawati 7,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ukombozi, James Mulokozi, alisema anatambua changamoto hiyo na amekuwa akifanya juhudi kusaka wadau ili kushirikiana kupata ufumbuzi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, alisema kutokana na eneo hilo kuwa na makazi mapya idadi ya wanafunzi inaongezeka na kwamba inaitajika kasi ya kuongeza madawati ili kuwawezesha wanafunzi hao kupata masomo kwa utulivu.

**ATHARI KISAIKOLOJIA**

Mwanasaikojia tiba, Saldin Kimangale, alisema mwanafunzi anayekaa chini wakati wa masomo anaweza kupata changamoto iwapo kuna wengine wanakaa kwenye dawati na akijilinganisha anaathirika kisaikolojia.

"Kukaa chini au kwenye dawati tunasema ni vichocheo vya kimazingira, lakini ili vifanye kazi utamaduni na ada za watu huzingatiwa sana. Iwapo shule nzima au darasa zima wanafunzi wanakaa chini bila shaka hakuna atakayeona kuwa ni tatizo," alisema.


**SERA ELIMU**

Sera inabainisha kuwa serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwapo wa miundombinu bora na toshelevu katika taasisi za elimu na mafunzo.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 inayosimamiwa na Wizara ya Elimu na Teknolojia kuna mgawanyo wa ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu kwa ngazi tofauti kuanzia wizara, mkoa, wilaya hadi serikali za mtaa.

Ofisa Elimu wa Halmashauri atakuwa na jukumu la kuandaa mipango na bajeti na kusimamia uendeshaji wa shule za elimu ya awali msingi na sekondari kwa kuzingatia maelekezo ya Sera.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawajibika pia kufanya uthibiti wa ubora wa elimu na mafunzo wa shule zilizoko katika maeneo yao kulingana na miongozo itakayotolewa na taasisi na mamlaka mbalimbali za kusimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini katika ngazi na mfumo husika.



# 400 kuajiriwa afya ya mama, mtoto

**Na Allan Isack,** ARUSHA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inakamilisha mchakato wa kuajiri watumishi 400 wa afya kupitia mradi wa kuboresha afya ya mama na mtoto nchini katika mwaka ujao wa fedha wa 2024/25.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, anayeshughulikia Afya, Dk.Wilson Mahera aliyasema hayo jana alipofungua mafunzo ya uongozi, menejimenti na utawala jijini hapa kwa waganga wakuu 53 wa wilaya za mikoa ya Tanga na Arusha.

"Tunajua kuna upungufu wa watumishi katika kada hii ya afya, lakini kuna mapango wa kuajiri wahudumu ngazi ya jamii na kwa kuanzia tutaanza na mikoa 10, tunachosubiri ni kupata kibali," alisema na kufafanua:

"Wanapoajiriwa, watumishi hao hawatakuwa wanafanya kazi moja moja watakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa magonjwa ya malaria, lishe, magonjwa ya kuambukiza na yasiyokuwa ya kuambukiza."

Alisema pamoja na kuajiri watumishi hao kwa mkataba wa miaka miwili, serikali pia itahakikisha inaongeza vifaa tiba na dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini ili kuboresha huduma za matibabu kwa wananchi.

Awali, naibu katibu mkuu huyo, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo na kuwapa stadi za kuwa uongozi bora waganga hao wa kusimamia huduma za afya kwenye sehemu zao za kazi.

"Ili kufikia hatua ya kutoa huduma bora za afya ni lazima tuwe na uongozi bora katika kusimamia rasilimali watu, fedha na kupanga mipango. Mafunzo hayo yatakwenda kuleta matokeo chanya kwa watumishi wa kada hii," alisema Dk. Mahera.

Aliwataka waganga wakuu wa wilaya kuwashirikisha watumishi walioko chini yao kusimamia rasilimali na mipango ili kuwaongezea morali ya kufanya kazi.

Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Watumishi wa Afya Arusha (CEDHA), Dk. Johannes Lukumay, aliipongeza serikali kwa kuwekeza zaidi Sh.trilioni 6.7 katika sekta ya afya kuimarisha miundombinu, vifaa tiba, dawa na kusomesha madaktari bingwa na bobezi.

Kwa mujibu wa Lukumay, mafunzo hayo yamefadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa lengo la kujenga uwezo wa timu za usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani, akimwagilia maji mti aina ya mchungwa alioupanda katika Shule ya Sekondari Pande, jijini Tanga juzi, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# James Mbatia avunja ukimya

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa zamani wa Chama cha NCCR Mageuzi, James Mbatia, amevunja ukimya baada ya kutosikika kwa zaidi ya miaka miwili na nusu tangu alipovuliwa wadhifa huo wa chama hicho Septemba 24, mwaka 2022.

Mbatia amejitokeza hadharani, akisema ukimya wake katika medani ya siasa za upinzani nchini, umemfanya apate nafasi ya kujifunza, kusikiliza na kujiuliza alikosea wapi, au alikokuwa sahihi.

Akizungumza jana na kituo kimoja cha televisheni mtandaoni, mwanasiasa huyo mkongwe alisema kuwa: "Kujifunza kwangu, kusikiliza na kujiuliza tena, mimi mwenyewe napata amani ya ndani zaidi, nastawi zaidi na kujiuliza labda nilikosea au nilikuwa sahihi. Tuseme ni historia ya mwanadamu.

"Nimekaa kimya ili kujifunza kwa sababu kusikiliza pia ni jambo la heri. Katika kusikiliza kwa makini nimejifunza mengi zaidi kuliko hata nilivyokuwa ndani ya mfumo. Kwa sababu unavyokuwa pembeni unapata nafasi ya kutafakari na kusikia kwa wenzako wanasema nini," aliongeza. Alisema amejifunza kubwa kuliko yote, angependa kutumia taaluma ya masuala ya majanga.

"Inabidi ukishakuwa na chemsha bongo ya maeneo mbalimbali unagawanya ile chemsha bongo, wengine wanaita classification," alisema.

Kwa mujibu wa Mbatia, anachokifanya kwa sasa ni kuangalia ubora wa yanayozungumzwa juu yake, masuala ya kisiasa yanayogusa muktadha mzima wa siasa ya Tanzania, au yale unayoyaona katika jamii.

"Na ukubwa wa jambo lenyewe na kiitikio chake kiko namna gani, mitigation yake iwe ya namna gani (usuluhishi), kinga yake au tiba yake iwe ya namna gani."

Kuhusu mifumo, Mbatia ambaye aliiongoza NCCR Mageuzi kwa zaidi ya miaka 20, ameeleza kuwa kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia ya dunia ya leo, kuna mahali teknolojia inafanya kama taifa wanakosa kusikilizana.

Alienda mbali zaidi kwa kusema mfumo ambao unamsaidia mwanadamu aweze kujitambua ni wa elimu.

Alifafanua kuwa mfumo wa elimu wa Tanzania kwa kiasi kikubwa ukiangalia wale watoto wanaoanza darasa la kwanza ni karibu asilimia 97, ambayo ni hatua kubwa taifa limepiga.

Alisema kati ya hao, wanaomaliza darasa la saba ni karibu asilimia 58 na kwamba jambo la kujiuliza asilimia 39 ya hao wasiohitimu elimu ya msingi inapotelea wapi.

"Lakini wanaoenda sekondari ni asilimia 28, wanaoenda vyuo vikuu ni asilimia tano. Wale wanaotoka vyuo vikuu wakaongoze wale wengine asilimia 92 waliobaki mitaani huko, hatuko vizuri," alisema Mbatia.

Septemba 24, 2022 ilitolewa taarifa inayoeleza kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa NCCR Mageuzi, walipitisha azimio la kumvua uenyekiti wa chama hicho wakati huo Mbatia na kumfuta uanachama.

# Ruksa kusafirisha mazao Bandari Tanga

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WIZARA ya Kilimo imetoa kibali cha kuanza kutumia Bandari ya Tanga kusafirishia mazao ya kilimo kutokana na kukidhi viwango vinavyostahili.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani aliyasema hayo kwenye kilele cha Siku ya Mazingira Duniani iliyofanyika katika Kata ya Pande jijini hapa.

Dk. Buriani alisema kuwa hatua hiyo ya wizara, imekuja kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa katika bandari hiyo.

Alisema maboresho hayo yameendelea kupanua wigo wa usafirishaji wa mizigo na kuongeza shehena inayoingia siku hadi siku katika bandari hiyo.

"Kwa sasa Bandari ya Tanga siyo saidizi bali ni bandari yenye viwango vyote vinavyostahili na inayojitegemea kwa nafasi yake," alisema na kuongeza:

"Wenzetu wa Wizara walikuja wakakagua bandari na wametupa cheti rasmi, sasa bandari yetu itatumika kusafirisha mazao ya kilimo ili vitu vyote viende sawa kunatakiwa kuwe na uratibu mzuri. "

Alipongeza usimamizi wa Simba Bingwa na kampuni zake kwa kuendelea kusimama mikataba ya usafirishaji majini kwa kuzingatia utoaji wa taarifa kuhusu bidhaa zinazosafirishwa ili kuepuka mchanganyiko wa kemikali na bidhaa nyingine.

Dk. Buriani, alisema upo mkataba kuhusu usafirishaji wa bidhaa zenye madhara na hilo linatekelezwa na kampuni hiyo wanapotaka kusafirisha lazima watoe taarifa kwa bandari.

"Hii inasaidia kutoleta madhara wakati wa upakuaji na pia kuwa na umakini zaidi, lakini kwa hili niwapongeze sana kwasababu wameonesha kusimama kidedea kutumia Bandari ya Tanga," alisema.

Alisema ili kutunza mazingira na kuondokana na mabadiliko ya tabianchi, kila mmoja anapaswa kutumia mazingira kwa kupanda miti kwa manufaa ya vizazi vya sasa na baadaye.

Mkurugenzi wa Simba Solutions, Ally Dewji, alisema kampuni hiyo imeanzisha kitengo cha Simba Terminajs kwa lengo la kufanya utafiti wa soko ili kuwekeza katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) za mtiririko wa ugavi.

"Utafiti wetu ulionesha kutakuwa na mapinduzi makubwa katika uchumi wa Mkoa wa Tanga, hususan mnyororo mzima wa thamani kupitia mshorona mpya ambao kwa sasa unajulikana kama Tanga Korido," alisema.

Dewji, alisema takwimu zinaonesha kuwa mwaka jana bandari hiyo ilihudumia meli 19, kati ya hizo, tano zilisimamiwa na Simba Terminals sawa na asilimia 26 ya meli zote zilizohudumiwa bandarini hapo.

"Kuendelea kupokea meli kupitia bandari hii kumeleta matokeo chanya ya uchumi katika Mkoa wa Tanga na nchi kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na ukuzaji wa ajira kwa vijana wa Kitanzania," alisema.

Alisema kila meli zinapotia nanga bandarini hapo, wamekuwa wakiajiri vijana kuanzia 250 hadi 300 kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali.





# KACU kujenga kiwanda cha mafuta

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) mkoani Shinyanga kinatarajia kujenga kiwanda cha kukamua mafuta ya mbegu za pamba ili kuinua maisha ya wakulima.

Mwenyekiti wa KACU, Emmanuel Nyambi, alisema kuwa wana mikakati ya kuhakikisha mkulima anarudi katika kilimo cha pamba baada ya wengi wao kuachana nacho kutokana na kukataa tamaa kwa kuwa ndiyo mkombozi wao na kupata faida mara mbili zaidi.

"Kiwanda hiki tunakijenga hapa hapa kwa sababu tuna eneo kubwa na fedha za ujenzi wa mradi huu zinatokana na mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), shughuli hizo tutaanza msimu ujao, faida itakayopatikana baada ya kutoa fedha za uendeshaji itarejeshwa kwa wakulima wetu," alisema Nyambi.

Chama hicho kilianza kununua pamba kwa wakulima msimu wa 2019/20 na kulipa malipo ya pili Sh.40 kwa kilo sawa na Sh.milioni 90 walizowalipa wazalishaji hao, hivyo kuongeza ushindani wa bei na kampuni zingine zaidi ya bei iliyokuwa imetolewa na serikali.

Alisema mkakati wa chama hicho ni kuhakikisha ushirika unamnufaisha kila mkulima mwanachama, kuongeza uzalishaji wa zao hilo ambalo bei yake inategemea Soko la Dunia.

"Msimu wa mwaka 2019/20 tulinunua pamba kilo moja kwa Sh.920 kulinganisha na bei iliyokuwa imetolewa na Serikali ya Sh.820, wa 2021/22 tulinunua kilo milioni 3.469 kwa bei ya Sh.1,825, huku bei elekezi ya serikali ilikuwa Sh.1,456," alisema Nyambi.

Mwenyekiti wa Amcos ya Uyongo, Maganga Masanja, alisema kiwanda hicho kitasaidia kuongeza ushindani wa bei.

# 'Samaki Ziwa Victoria wana plastiki'

**Na Aneth Ntungo,** SAUT

ASILIMIA 20 ya samaki katika Ziwa Victoria wana chembechembe za plastiki kutokana na kukithiri kwa uchafuzi wa mazingira na utupaji wa taka ndani ya ziwa hilo, imeelezwa.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la Synergistic Globe, Vitus Medard wakati wakifanya usafi wa mazingira kwa kukusanya taka katika Kata ya Luchelele jijini Mwanza, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

"Tafiti zilizofanya na Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) katika Ziwa Victoria zilibaini kati ya samaki watano, mmoja ana chembe za plastiki zinazotokana na baadhi ya wananchi ndani ya jamii wanatupa uchafu pembezoni na ndani ya ziwa, hali hii inahatarisha usalama wa samaki na mazalia ya viumbe hai," alisema Medard.

Alisema shirika hilo limeanzisha mradi unaojulikana kwa jina la Marafiki wa Ziwa Victoria kwa lengo la kusimamia, kuelimisha, kuhimiza uhifadhi wa vyanzo vya maji na kupunguza uchafu katika maeneo hayo, hususani vyanzo vinavyotiririsha maji ziwani humo, ikiwa ni kutokomeza uchafu wa taka ngumu na plastiki. Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Meneja wa Mamlaka hiyo Kanda ya Nyegezi Imrani Swai Kanda ya Nyegezi alilipongeza shirika hilo kwa kazi wanazofanya na kuwasihi waendelee na juhudi za kutokomeza uchafuzi wa mazingira unaotokana na jamii.

Mratibu wa mradi wa marafiki wa ziwa hilo, Tabu Manyama, alisema kila mwananchi ana jukumu la kutunza mazingira yanayomzunguka ili yawe endelevu kwa jamii ya sasa na vizazi vya baadaye.

Wakati wa maadhimisho hayo, Synergistic Globe ilifanya usafi kwa kuokota taka za plastiki, kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kupanda miti katika Kituo cha Afya cha Nyegezi.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Mhandisi Yusuph Katopola (katikati mwenye suti), akitoa maelezo kwa Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kuhusu utekelezaji wa mtambo wa tope kinyesi katika eneo la Mwagala juzi. Mitambo kama hiyo inatarajiwa kujengwa katika maeneo ya Ihapa, Kituli na Mwamakalanga, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mradi kumaliza shida ya maji Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MRADI wa majisafi na usafi wa mazingira unaotekelezwa katika Manispaa ya Shinyanga unatarajiwa kutatua kero ya maji kwa wananchi ambao hawajafikiwa kabisa na huduma hiyo, imefahamika.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Mhandisi Yusuph Katopola wakati akizungumza na madiwani wa Manispaa hiyo na wadau wa maji juu ya utekelezaji wa mradi huo.

Katopola, alisema utekelezaji wake umeanza kwa hatua za awali kwa kukarabati miundombinu na kupanua mtandao wa maji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakazi 282,698 wakiwemo 189,580 wanaopata huduma ya majisafi na salama sawa na asilimia 67.1.

"Wastani wa mahitaji ya maji kwa wananchi ni mita za ujazo 19,288, tunazosambaza kwa siku ni mita za ujazo 14,936, hii inatokana na miundombinu waliyonayo, kupitia mradi huu wananchi wote watapata majisafi na salama," alisema Katopola.

Mratibu wa Miradi wa SHUWASA, Mhandisi Willfred Julius, akiwasilisha taarifa ya utekelezwaji wa mradi huo, alisema serikali ya ilisaini mkataba wa mkopo wa masharti nafuu na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD)kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira. Alisema mradi huo umelenga kuboresha miundombinu, ujenzi wa mitambo ya kuchakata tope, kinyesi na ujenzi wa vyoo 36 maeneo ya shule, soko, vituo vya afya na kufanya upanuzi wa chanzo cha maji bwawa la Ning'hwa ili liwe na uwezo mkubwa wa kutoa ya maji.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Said Kitinga, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Mtatiro, alipongeza SHUWASA kwa kushirikiana na madiwani na wadau wa maji ili kuboresha maisha ya wananchi.

# Bomba la mafuta ghafi lashusha neema kwa wananchi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

ZAIDI ya wananchi 9,822 wa mikoa minane nchini wamelipwa fidia kupisha ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga.

Akizungumza katika warsha ya waandishi wa habari mkoani Geita, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Mradi huo Afrika Mashariki (EACOP) Tanzania, Abbas Nassoro alisema kuwa mradi huo unatekelezwa na Serikali chini ya Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) kwa kushirikiana na wadau wengine, ikiwamo Serikali ya Uganda.

Nassoro alisema kuwa wananchi hao wamelipa fidia za fedha na kujengewa nyumba baada ya kuguswa na mradi huo.

Alisema mradi huo uko kati hatua za kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi hao na kwamba umefikia asilimia 99 kwa kujenga nyumba 339 kwa upande wa Tanzania.

Mratibu wa mradi huo Mkoa wa Geita, Moses Msofe, alisema mradi huo umewajengea nyumba za waliopisha mradi katika wilaya za Mbogwe, Bukombe, Chato na Geita .

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Mradi huo, Catherine Mbatia, aliwataka waandishi wa habari mkoani humo kuwaelimisha wananchi umuhimu wa mradi huo kwa manufaa ya Afrika Mashariki.

Catherine, alitaja mikoa nchini ambako mradi huo kwa asilimia 80 umepita kuwa ni Geita, Shinyanga, Singida,Tabora, Manyara, Dodoma na Tanga.

Alisema wananchi wa vijiji vinavyopitiwa na mradi huo wamenufaika kwa kupata ajira za muda mfupi na za kudumu.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Geita, Renatus Masuguliko, alisema mafunzo hayo yata wasaidia waandishi wa habari mkoani hapo kuwa na taarifa sahihi za mradi huo .



Ukurasa 12

**Miezi minne ziara zake maalum RC Chalamila, akitakatisha 'uvunguni'**




Ukurasa 13

Watendaji serikali, tuwe wa kwanza vita vya mikopo 'kausha damu' tuliko

BUFE
IJUMAA JUNI 7, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

BAADA WAZIRI KUTANGAZA KAMPENI...

**Taasisi Wizara Fedha yafafanua elimu ya uwekezaji kwa wastaafu**

MTAJI WA KIMATAIFA...

# Undani wa Diplomasia Uchumi nchini, anachokumbatia muumini Dk. Samia

**Na Mwandishi Wetu**

DIPLOMASIA Uchumi umekuwa mwelekeo mpya kisera nchini kimataifa. Imezaliwa na kiutawala duniani, baada ya kifo cha vita baridi duniani, kati ya ngome ya Magharibi na Mashariki, sambamba na migogoro yake kimataifa.

Hali hiyo imeyafanya mataifa kutafakari namna bora ya kusimamia maslahi yake, katika dunia inayoangazwa na mwelekeo wa kunufaika na soko lililoko kimataifa.

Kwa kutambua hilo, serikali nchini ikaandaa Sera ya Mambo ya Nje inayozingatia Diplomasia ya Uchumi, ili kupata maslahi ya msingi ya taifa na kuwawezesha wananchi wake kupiga hatua za kimaendeleo.

Sera ya Mambo ya Nje imezingatia kupanga, kukuza na kulinda maslahi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa namna endelevu, kuhakikisha uhusiano mzuri wa Tanzania na mataifa mengine.

Hata taifa lilipofika uongozi wa Awamu ya Sita, miaka mitatu na robo sasa, ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, msomi wa uchumi na utawala, amedumu nao akiwa muumini wa vitendo, mifano hai ikitingwa na madhumuni na vitendo vya ziara zake kimataifa, ikiwamo wiki iliyopita nchini Korea Kusini.

Msingi wa Diplomasia Uchumi nchini, kiuchumi inatajwa kuchangia kuharakisha utangamano kisiasa na kiuchumi na kijamii, ukiweka mazingira muhimu yanayoiwezesha Tanzania kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kikanda na kimataifa.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki, January Makamba. **PICHA: MAKTABA**

Muumini wake, Rais Dk. Samia, ndani ya ziara zake zote, amekuwa mshiriki hai, kama vile alivyokuwa nchini Ufaransa hivi karibuni, akiongoza kikao na wiki iliyopita akawasilisha mada kikaoni nchini Korea Kusini.

Ndio falsafa sasa inayoegemewa na nchi nyingi duniani, zikihimiza majukumu ya kikanda kama Tanzania ilivyo na uanachama wea Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ikiwa mwasisi na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrrika (SADC).

Kwa mujibu wa jarida la Wizara ya Mambo ya Nje, mwaka 2021, inanukuu: "Serikali ya Awamu ya Sita, imeendelea kujikita zaida kwenye Diplomasia ya Uchumi.

"Ni mkakati mojawapo wa nchi kushirikisha mataifa ya kigeni kujinufaisha kiuchumi katika sekta za biashara na uwekezaji, kilimo, utalii, elimu, afya, mikopo ya riba nafuu na kupata teknolojia ya kisasa."

Wiki iliyopita, Rais Dk. Samia alirejea nchini na fedha za mkopo nafuu kutoka Korea Kusini Sh. Trilioni 6.478 (Dola za Marekani bilioni 2.5) mbazo zinalenga kugharamia miradi ya elimu, afya na miundombinu.

Mafanikio yailiyoko hadi sasa ni kwamba, taifa limeshasonga mbele kutekeleza Diplomasia ya Uchumi, ikiwa na mfano wa mafranikio kibiashara na taifa la Saudi Arabia, kukiwa na milolongo ya miradi iliyobuniwa na kuwekezwa nchini.

Vilevile katika taifa kama China, Tanzania imekuza ushirikiano wa namna hiyo, kibiashara, uwekezaji, fedha, kilimo, nishati, viwanda, utalii, madini na miundombinu, vyote vikidhi viwango na ubora unaokubalika katika soko la kimataifa.

### ALIPOFUNGUKA BUNGENI

Rais Dk. Samia akihutubia Bunge Aprili, 2021 jijini Dodoma, akaahidi amefanya kufanya mageuzi katika uhusiano na ushirikiano kimataifa, kwa kutekeleza shughuli za kidiplomasia kwa ufanisi zaidi, ili kuendana na utekelezaji wa sera ya Diplomasia ya Uchumi.

Akasema kuwa, serikali yake imejipanga kuendeleza uhusiano na ushirikiano na mataifa mengine, pia taasisi za kidunia, kutekeleza shughuli za Kidi- plomasia kuendana na Sera ya Diplomasia ya Uchumi.

"Tumekusudia kuimarisha na kukuza Uhusiano na Mataifa mengine pamoja na jumuiya za kikanda na Taasisi za Kimataifa," akasema, akitaja baadhi ya njia zake ni katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pamoja na ofisi za ubalozi zetu zilizoko nchi mbalimbali duniani, kwa kuajiri watumishi wenye sifa na weledi wa kazi na kusambaza vitendea kazi, pamoja na kutumia kiuchumi.

Akafafanua, katika madhumuni ya kuwezesha utekelezaji mzuri wa Diplomasia ya Uchumi, serikali imekusudia kuboresha na kusimamia majengo na viwanja ambavyo ni mali ya Tanzania vilivyoko nje ya nchi.

Rais akanena: "Naomba kuwahahikishia kuwa tutafungua na kuanzisha pia Balozi mpya, Konseli pamoja na Vituo vya Biashara kwenye nchi na miji ya kimkakati ili kutangaza vivutio vyetu vya utalii, ku- vutia uwekezaji na kutafuta masoko ya bidhaa zetu."

"Tutaendelea kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kimataifa, ikiwamo ushiriki wetu kwenye kulinda amani duniani. Tunakusudia pia kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwa- ka 2000 ili iendane na mahitaji ya sasa ya dunia," anaongeza Rais Dk.Samia.

UCHUMI

# Miezi minne ziara zake maalum RC Chalamila, akitakatisha 'uvunguni'

## • Ahitimisha akisikiliza kero zao hadi giza lilipoingia

**Na Pilly Kigome**



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alipokutana na wakazi katika ziara yake kuwatembelea wakazi wa Mchikichini Kota, Ilala.
**PICHA: PILLY KIGOME**

ILIKUWA Februari 19, mwaka huu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alipoanza ziara yake kuzunguka halmashauri zote tano na majimbo yanayopatikana katika halmashauri hizo kwa lengo la kusikiliza kero za wananchi wake katika mikutano ya hadhara iliyofanyika maeneno tofauti na azipatie ufumbuzi.

Mbali na kusikiliza kero na dukuduku kutoka kwa wananchi, lengo la ziara pia lilikuwa kutembelea miradi inayotekelezwa katika majimbo husika kuona kasi na utekelezaji wake.

Akiwa jimboni Temeke, alitembelea mradi wa kupunguza makali ya ukosefu wa umeme pamoja na kuboresha miundombinu mkoani Temeke mradi unaogharimu shilingi bilioni 16, mradi utakaoleta umeme wa uhakika wa kutokukatika katika wenye ujazo wa KV 132 kutoka Ilala hadi  Kurasini ukiopita chini ya ardhi watekelezaji ni kampuni binfasi, unatajwa kukamilika Machi mwaka huu.

Mku wa Mkoa alitembelea mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Lumo iliyopo Yombo na hapo akabaini 'madudu' ya wizi na ubadhirifu kwa baadhi ya watendaji.

Pia, alizindua mradi wa shule mpya ya msingi ya Ushirika iliyogharimu jumla ya shilingi milioni 475 iliyopo kata ya Yombo Vituka.

Awali alitembelea mradi wa Shule ya mazoezi ya Chang'ombe iliyopo kata ya Migulani katika Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu cha DUCE mradi huo ulikuwa na jumla ya madarasa saba na matundu kumi ya vyoo.

Vilevile, alikagua mradi wa ujenzi wa barabara ya mita 350 iliyopo mitaa ya Wailesi na Kitomondo, Temeke   ambako katika mradi hiyo, tayari fedha za DMDP zimeshapokewa kuendeleza mradi huo ikiwamo kutengeneza na kukarabati mitaro iliyopo katika mradi huo.

Akiwa katika mkutano wa hadhara Lumo Sheli mwananchi walipoanza kutoa kero zao mdokeza mkuu huyo kuna wizi umefanyika katika mradi wa Shule ya Sekondari Lumo, RC Chalamila aliwaagiza Kamanda wa Polisi na TAKUKURU kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo ndani ya saa 24 na ikithibika watu hao watachukuliwa hatua za kisheria haraka.

Waliodaiwa kuhusika na wizi huo idadi yao walikuwa saba wamedaiwa kuiba vifaa vya ujenzi wa shule hiyo mpya inayoendelea kujengwa yenye idadi ya vyumba 32 vya madarasa, ofisi 16 za walimu na matundu 96 ya vyoo kwa fedha za maendeleo ya elimu zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kutoka serikali kuu na mapato ya ndani. Mradi ulianza Januari mwaka huu.

Ziara iliendelea katika Halmashauri ya Kinondoni na huko alitembelea miradi ukiwamo Shule ya Serikali ya Chekechea na Msingi ya mchepuo wa Kiingereza iliyopo Kigogo, alitembelea mradi wa ujenzi wa jengo la ghorofa moja cha Kituo cha Afya Kinondoni.

Pia, alitembelea mtaa wa viwanda eneo la Mikocheni kwa mwekezaji wa raia wa China, akizalisha chupa za plastic zinazosafirishwa nje ya nchi.

Baadaye, Chalamila aliweza kusikiliza kero za wananchi huko katika viwanja vya Mwananyamala Mwinjuma na Mabwepande, wilayani Kinondoni.

Akiwa Mabwepande, mengi yalijitokeza huku wananchi kupiga mayowe mbele ya mkuu huyo kwa kumwomba wapatiwe shule ya msingi katika kata hiyo ambayo hakuna watoto wanakwenda umbali mrefu kufata huduma hiyo.

Wananchi hao walipiga mayowe kwa kusema kuwa kuna eneo kubwa kupitiliza ambalo halitumiki linalomilikiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), wakitaka wajengewe shule hiyo. Pia wakaomba wapatiwe eneo la maziko, kwa kuwa hawana wanafuata umbali mrefu huduma hiyo.

Akiwa katika Manispaa za Ubungo na Kigamboni, nako akakagua miradi  na kusikiliza kero mbalimbali za wananchi, ikiwamo za maji, miundombinu, ardhi na ukatili na kuzipatia ufumbuzi katika ofisi zake.

RC Chalamila akahitimisha ziara yake katika Halmashauri ya Jiji la Ilala, alikotumia siku tatu kutembelea majimbo matatu; Ukonga, Ilala na Segerea, akikagua miradi na kusikiliza kero za umma.

Ni safari iliyoanza na Jimbo la Ukonga na baadaye akasikiliza kero za wananchi katika Uwanja wa Pugu Kona na ziara ikaendelea siku iliyofuata jimboni Ilala, alikokagua miradi mbalimbali, ikiwamo kutembelea Shule ya Sekondari Benjamini Mkapa.

Hapo akakagua mradi wa jengo jipya la vyumba vya madarasa na ukumbi wa mikutano wenye thamani ya shilingi milioni 800.

Akiwa hapo, Chalamila akaelezwa kutofurahishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo, akitamka anaona linanasuasua.

Pia, akatembelea mradi wa Kituo cha Afya Mchikichini, utakaogharimu zaidi ya shilingi bilioni tano, akibaini matofali yanayotumika katika ujenzi huo hayakuwa katika viwango stahiki.

Ni mradi anaodai unasuasua, baada ya mkandarasi aliyepo sasa kusuasua na ujenzi, akiurithi mradi kutoka kwa mkandarasi wa awali, aliyeshindwa kuendelea na ujenzi kwa kukosa fedha, licha ya kuwa alipatiwa fedha ya awali zaidi ya shilingi bilioni moja.

Hapo akatoa agizo kwa viongozi wanaotoa tenda za miradi katika halmashauri hiyo, kuwa makini na wanaowakabidhi miradi, akiwataka watumie sifa stahiki na si kupeana tenda kwa kujuana, kunakochangia madhara katika miradi hiyo.

Awali alikagua mitaro iliyoziba kando mwa barabara eneo la Posta, ambako akawaagiza wanaosha magari ya wanaoosha magari yao, kando mwa barabarani wasiendelee na shughuli hizo pembezoni.

Nako akaziagiza manispaa husika kuwatafutia sehemu stahiki na si kando mwa barabara. Baadaye akakagua barabara za watumiaji Mtaa wa Lindi Kata ya Gerezani, alikotajiwa ilikuwa kero. Baadaye akahitimisha na mkutano wa hadhara eneo la Ilala Kota na kupokea kero mbalimbali za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Siku iliyofuata, iliyoyoma katika jimbo la Segerea alikitembelea kiwanda cha Nondo cha Metro kilichopo Kiwalani kisha kuelekea Shule ya Sekondari Minazi Mirefu, alikoukagua mradi wa ujenzi wa ghorofa nne wa vyumba vya madarasa.

Baadae akaenda kukagua Kituo cha Afya Kinyerezi na kuhitimisha na kusikiliza kero za wananchi wa Tabata Kimanga, alikopatowa malalamiko mengi sana, Chalamila akidumu kuzisikiliza hadi muda wa giza.

# TRA mtaani 'kumuunga' Mama elimu risiti, kumtambulisha msuluhishi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAKATI Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatangaza kukusanya mapato ya kodi Sh. trilioni 21 hadi kufikia Aprili mwaka huu, sasa imekuja na rai ikiwakubusha Watanzania kwamba, ulipaji kodi unachangia kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa nchi.

Hapo inaelekeza rai yake kutaka Watanzania wajenge mazoea ya kudai risiti, hasa wanaponunua hata vitu vidogo kutoka madukani.

Waziri wa Fedha. Dk. Mwigulu Nchemba, akitoa taarifa ya mapato na matumizi katika Bunge linaloendelea jijini Dodoma, kwa wizara mbalimbali.

Inafafanuliwa kwamba, ukusanyaji huo unaoonyesha jinsi ulipaji kodi mzuri, unavyoweza kuongeza pato la uchumi la taifa.

Uhalisia uliopo, bado kuna kasumba kubwa kwa watu kuwa wavivu wa kudai risiti wanaponunua bidhaa, suala linalochangia kwa kiasi kikubwa kupunguza mapato ya nchi.

Kinyume chake, mtu anatakiwa kudai risiti popote pale unapotoa pesa yake kununua bidhaa au huduma. Akifanya hivyo, anakuwa tayari amesaidia kwa kiasi kikubwa kuchangia uchumi wa taifa.

Kuna uzoefu katika baadhi ya nchi jirani ukanda wetu wa Afrika Mashariki ni ngumu kununua bidhaa au huduma, bila ya kupata risiti. Hivyo, inajenga utashi hata nchini inatakiwa kujenga mazoea hayo kudai risiti pale mtu anapoenda dukani kununua bidhaa yoyote ile.

Ndio maana wenye dhamana, TRA wamekuwa wako katika kampeni kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kudai risiti, pale unaponunua bidhaa ua huduma, pia analipa kodi, hoja ambayo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akisisitiza umuhimu wake.

Haki ya kudai risiti ni dhaya na maendeleo na kuelimika, huku akijenga uchumi wake. Kwenye vitu mbalimbali vya mahitaji ya binadamu unavyonunua, ili kuhakikisha kila mmoja anachangia uchumi wa taifa risiti ina maana kubwa.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Mlipakodi wa TRA, Hudson Kamoga, anasema suala la ulipaji kodi likizingatiwa, lina nafasi kutanua uchumi wa nchi.

Anasema wengi wa jamii wamekuwa wagumu kudai risiti pale wanapouziwa bidhaa kitu ambacho sio sahihi wanachopaswa kufanya ni kudai risiti ili wawe salama na bidhaa zao.

Kamoga anasema, lengo lao ni kuona watu  wanajenga mazoea ya kudai risiti wanaponunua bidhaa, pia kulipa 'kodi ya kichwa' kwa kila mmoja.

"TRA tunaendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa jamii. Lengo letu ni kuona watu wote wanajua mini umuhimu wa ulipaji kodi ya taifa Kwa kila mmoja,"anasema Kamoga.

Anafafanua kuwa hadi sasa wanachokifanya TRA kila kukicha ni jitihada za kutoa elimu kwa umma, wanajamii kuhusu ulipaji kodi kwa jamii kulivyo muhimu kitaifa, kwa sababu inatanua uwezo wa taifa kujimudu katika kutimiza na kuhudumia mahitaji yake. Pia, anasema hivi sasa wanaendelea wanamfikia kila mtu elimu ya wajibu wao kulipa kodi.

Waziri Fedha, Dk. Mwigulu amekuwa akiwasisitiza TRA kudai kodi, ikienda sambamba na utoaji elimu ya kodi kwa umma.

**RC DODOMA ANENA**

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, anasema Watanzania wanatakiwa kulipa kodi, ikiwa ni takwa la kisheria katika nchi zote duniani yenye maendeleo, katika mustakabali wa kukuza uchumi wake.

Senyamule, anasema pamekuwapo fursa ya kulipa kodi, inapaswa wananchi, waiwajibikie na huduma serikali ni haki yao.

" Kulipa kodi ni jambo la kihistoria na kiimani pia, kwani hakuna nchi inaweza kuendelea bila ya kodi," anasema Senyamule, akiwahimiza wakazi wake kulipa kodi kwa hiari, wasisubiri nguvu kutumika.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabir Shekimweri, amemshukuru Rais katika kwa kusukumwa kuanzisha chombo kinacholea suluhu katika migongano ya makadirio ya kodi.

Kaimu Ofisa Msuluhishi wa Makadirio ya Kodi, Godwin Barongo, anasema dhumuni la kuanzishwa Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi, ni kushughulikia malalamiko na taarifa za kodi, yaliyoko kisheria.

Aidha, anasema kuanzishwa ofisi hiyo, kunatarajiwa kwamba kutatoa ufanisi na kupunguza gharama za ukusanyaji mapato.

Kampeni iliyoko sasa ni ya utoaji elimu kwa umma na kuitambulisha Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi Tanzania (Tax Ombudsman Service Tanzania - TOST) ikiongozwa na kaulimbiu, "Kataa ukwepaji kodi, kataa kodi za dhuluma".

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Watendaji serikalini tuwe wa kwanza vita vya mikopo 'kausha damu' tuliko






**NA ADAM FUNGAMWANGO**

AKIWA bungeni jijini Dodoma, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Lameck Nchemba, aliahidi kupambana na mikopo isiyo rafiki kwa Watanzania, maarufu 'kausha damu.'

Alikiri kuwa aina hiyo ya mikopo hutolewa na taasisi ambazo hazina leseni ya Benki Kuu na serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuzuia mikopo hiyo, ikiwa ni pamoja na kuzitaka kampuni za simu kuhakikisha mifumo yao haitumiki katika shughuli zozote zinazohusiana na mikopo hiyo, ikiwa pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ili kuepukana na mikopo hiyo.

"Vile vile, serikali inaendelea kuwafuatilia wahusika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi ya wanaokiuka taratibu zilizowekwa" alisema Dk. Nchemba.

Ni kweli kabisa hivi sasa kuna mikopo mingi kupitia simu za viganjani ambayo hutolewa kwa ushirikiano kati ya taasisi zilizopewa leseni kihalali, ambazo zinafuata kampuni za simu zilizopewa leseni ya mifumo ya malipo.

Ushirikiano huo unaainisha majukumu ya kila mtoa huduma ambako taasisi zinazotoa mikopo hutoa mikopo hiyo kulingana na sheria na kanuni za leseni za utoaji mikopo huku kampuni za simu zikitoa mifumo.

Lakini kwa sasa kuna vikundi ambavyo havijasajiliwa na watu binafsi ambao wamejiingiza kwenye kazi hiyo ya kutoa mikopo kwa wananchi.

Ninavyojua, serikali ina nia njema tu kwa wananchi, hivyo haiwezi kuweka masharti magumu ya mkopaji kiasi kwamba kama akishindwa kwa muda husika, basi ataifishwe vitu vyake, samani, mali, au kitu ambacho kinamwingizia pesa, au kumfanya kuendesha maisha yake.

Lina utaratibu ambao unafanya kumuumizi mkopaji, na kumpa fursa ya kuwa na hamu au shauku ya kukopa tena.

Pamoja na nayo, kama nilivyosema, vipo vikundi visivyosajiliwa au watu ambao wanatoa mikopo hiyo mitaani na kwenye simu za mkononi.

Nimeshuhudia pale maeneo ya stendi Morocco, Dar es Salaam, kumebandikwa tangazo kabisa la mtu mmoja au kikundi ambacho kinakopesha fedha kuanzia Sh 10,000 mpaka 100,000.

Walengwa ni madereva na makonda wa daladala, ambao wanaambiwa kabisa kama wana shida ya kulipia leseni zao za udereva, au wanadaiwa, wanakaribishwa kukopa kwa ulipaji na masharti nafuu, huku wanaofanya hivyo wakiwa wameweka namba zao ili mkopaji awasiliane nao namnba mbili za simu zimewekwa, katika nguzo jirani na magari ya kwenda Bunju yanakopakia abriria.

Sidhani kama kikundi au mtu aliyeweka tangazo hilo ana leseni ya Benki Kuu. Kwanini kitu kama hicho kisiwe kwenye mfumo wa simu za mkononi, mwombaji afuate taratibu zile zile, badala ya kupiga simu moja kwa moja?

Ukiacha mbali hilo, huko mitaani ndiyo kabisa. Utakuta mtu na kikundi kikipita mitaani, tena vingine viwahusisha hata Mwenyeviti wa Serikali za Mitaa au Wajumbe ili vipate kuaminika, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa havikusajiliwa na mikopo yao huwa ndiyo ile ambayo si rafiki, maarufu kama 'kausha damu.'

Watu wanakopa kutokana na umasikini, au mahitaji muhimu ya wakati ule, lakini baadhi yao hawana uhakika wa kulipa, kwa kutokuwa na vyanzo sahihi vya kuingiza vipato na mengine yanayofanana na hayo.

Matokeo yake wamekuwa wakipata usumbufu na kudhalilishwa wakati wahusika wanataka marejesho yao.

Kama Dk. Mwigulu ameshasema hayo, ni wakati sasa kwa wahusika wanaochukua hatua kufanya kazi hiyo ili kuendana na kile alichoanisha mwenyewe kule bungeni.

Mfano hao wanaotoa mpaka namba ili wakopaji wawapigie, sidhani kama ni ngumu kuwatia mbaroni.

Pia, kama alivyosema mheshimiwa, tunaweza kuzunguka kote huko, lakini elimu kwa wananchi ni muhimu.

Serikali itengeze kitengo cha kutoa elimu juu ya mikopo hiyo, na kuwataka wananchi wajielekeze kukopa kule ambako hawatopata matatizo, yaani kwa wahusika wenye leseni tu ili kuepuka kuchukulia mali zao, ikiwamo vitu vyao ndani kama televisheni, vitanda, magodoro, friji na vingine, ikiwamo kudhalilishwa utu wao.

Pia serikali ina wajibu wa kuwahabarisha wananchi wake na kuwaonya hata hiyo mikopo kutoka kwenye taasisi sahihi wafanyie vitu vya maana, kama biashara, kuongeza mitaji, kwenye kilimo, na siyo kwa ajili ya kufanyia sherehe, 'pati', kununua vitu kwa ajili ya kutunza, ngoma au nauli ya kusafiria kwenda kuwaona ndugu kwa sababu mwisho wa siku watashindwa kurudisha.

UCHUMI

BAADA YA WAZIRI KUTANGAZA KAMPENI...

# Taasisi Wizara Fedha yafafanua elimu ya uwekezaji kwa wastaafu

- Wanafunzi wasukwa kivyao, wabadilike

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Fedha, Dk.Mwigulu Nchemba, hivi karibuni amewaambia wabunge kuwa wizara yake inaendelea kupokea maoni na mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wadau, kuhusu umuhimu wa elimu ya huduma za fedha kwa umma katika kukuza shughuli za kiuchumi na ustawi wa jamii.

Dk. Nchemba aliyasema hayo Juni 4, mwaka huu bungeni jijini Dodoma, wakati akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/2025.

Anasema, kwa mwaka wa fedha uliopita 2023/24, wizara yake imeendelea kutekeleza mkakati wa utoaji elimu ya fedha vijijini, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Fedha kwa Umma ya Mwaka 2021/22-2025/26.

"Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na taasisi za usimamizi ikiwamo Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Dhamana pamoja na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, imeunda timu maalumu ya wataalamu kutoa elimu kwa umma, hususani vijijini," anasema Dk.Mwigulu.

Anaendelea: "Ni kwa utaratibu wa semina, warsha, makongamano, filamu, runinga, redio, mitandao ya kijamii na mafunzo kwa waratibu waliopo katika halmashauri zetu."

Dk. Mwigulu anasema makundi yaliyopewa kipaumbele katika zoezi hilo la elimu linaloendelea hivi sasa nchini nzima kwa umma, ni ya wajasiriamali wadogo, wanawake, vijana, watu wenye mahitaji maalumu na waajiriwa.

Kuna jitihada za kuhakikisha elimu ya fedha inaenea nchini nzima na wananchi wanapata fursa za kuwekeza na kuwa na matumizi sahihi ya fedha kwa ustawi wa jamii na familia zao.

Ndani ya wizara yake, watendaji wakuu kampuni ya UTT AMIS, kwa zaidi ya miaka 10 imekuwa ikitoa mchango mkubwa kwa Watanzania na taasisi za kimataifa katika kuchochea maendeleo na kukuza uchumi katika jamii na taifa kwa ujumla kwa kutoa elimu mbalimbali.

Hivi karibuni UTT AMIS wametoa mafunzo ya matumizi sahihi ya fedha kwa wananchi



Waziri wa Fedha na Uchumi, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha hoja bungeni. **PICHA: MTANDAO**

> **Mtu akiwekeza katika mifuko hii, tunao wataalamu ambao watawasimamia vizuri na kuhakikisha wanaelewa lengo na kupata faida stahiki.**

wa kada mbalimbali jijini Dar es Salaam, lengo likiwa kuwaelimisha umuhimu wa kuwekeza katika mifuko ya UTT AMIS kwa ajili ya kujiandaa maisha baada ya kustaafu.

"UTT AMIS imekuwa ni suluhisho, tumekuwa tukitoa mafunzo kila siku na kokote kwenye uhitaji tunakwenda na tunatoa mafunzo.Mafunzo haya ni bure," anasema Mbaga na kuongeza kuwa:

"UTT AMIS tunaendesha mifuko sita, kwa ajili ya uwekezaji, mifuko hiyo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Kujikimu, Mfuko wa Ukwasi na Mfuko wa Hatifungani.

"Mtu akiwekeza katika mifuko hii, tunao wataalamu ambao watawasimamia vizuri na kuhakikisha wanaelewa lengo na kupata faida stahiki," anasema.

Akizungumzia semina hiyo Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Daudi Mbaga, anasema katika maisha ya kufanya kazi kuna wakati mfanyakazi anastaafu, anaweza kuwa ukomo kwa mujibu wa sheria kwa maana ya kustaafu unapofika miaka 55 hadi 60 na kwa madaktari na maprofesa, miaka 65.

"Wakati mwingine si hivyo tu, unaweza kustaafu kabla ya umri huo, kwa mfano kampuni au taasisi imefilisika au wakati mwingine unaweza kustaafu kwa sababu ya afya.

"Hivyo, si lazima ufike wakati wakati huo. Kwa hiyo wakati unaanza kazi ujue siku moja utastaafu, basi kuna haja ya kujiandaa," anasema Mbaga.

Anaendelea: "UTT AMIS na Vertex tuliona kuna fursa ambazo zipo UTT AMIS, fursa ambazo ziko katika hatifungani za serikali na fursa kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam. Ni sehemu ambayo kwa kutumia fursa hizo linaweza kuwa suluhisho kwa maisha baada ya kustaafu."

Anaongeza kuwa Taasisi ya UTT AMIS, kwa kushirikiana na Taasisi ya Vertex, waliona haja ya kuandaa semina kwa wananchi kutoka kada mbalimbali, kwa ajili ya kuwapa elimu hiyo muhimu.

"Kama inavyofahamika mtu akipata elimu anakuwa na weledi kwenye jambo fulani hata kukabiliana nalo. Kwa hiyo ndilo kubwa ambalo limetuleta hapa," anasema.

Mbaga anafafanua kwamba, kwa upande wa mfuko ambao unapendwa na wastaafu wa Hatifungani, ambao una miezi kama 55 au 56 tangu ulipoanzishwa, hivi sasa unahudumia idadi kubwa ya wastaafu na una zaidi ya shilingi bilioni 600.

"Pamoja na hayo, wastaafu pia wako katika mifuko mingine kwasababu ukija pale UTT unachagua mfuko ambao unautaka. Kwa hiyo, tunaweza kusema mwitikio ni mkubwa na kwa sababu tu ya changamoto ambazo wakati mwingine ziko kwenye maeneo mengine, ambako wastaafu wangeweza kuwekeza.

"Unakuta mstaafu amefanya kazi miaka 30, hajawahi kufuga kuku lakini akipata fedha ya kustaafu unaenda kwenye kufuga kuku, wanampiga chenga au wakati mwingine hujawahi kumiliki daladala.

"Unapoenda kununua daladala, kwa sababu unahela baada ya muda mfupi unajikuta uko nje ya biashara matokeo yake unapata mfadhaiko au ukapoteza maisha," amesema Mbaga.

Katika muktadha huo, Ofisa Mwandamizi Idara ya Masoko na Mahusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, anaifafanulia Nipashe kwamba, elimu ya huduma za fedha kwa umma ina umuhimu, hapo akitilia mkazo unaoanzia wanafunzi ngazi ya msingi, ili kuzalisha kizazi chenye nidhamu ya matumizi ya fedha zao.

"Tumegundua watu wengi hawana utamaduni wa kuweka akiba au kufanya uwekezaji. Chanzo huenda ni msingi mbovu tangu mtu akiwa shule. Kama elimu ikitolewa kwa wanafunzi mapema, italeta matunda baadaye kwa mtu mmoja mmoja au taifa kwa ujumla," anasema Mwanga.

Anaongeza kuwa UTT AMIS, ina jukumu la kuanzisha na kuendesha mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa mujibu wa sheria ya masoko ya mitaji na dhamana ya mwaka 1994 pamoja na marekebisho yake na kanuni zake za 1997.

Anasema mbali na elimu kwa wanafunzi, pia wananchi wanapaswa kufahamu juu ya uwekezaji kwa ajili ya kutengeneza maisha ya baadae na katika kulizingatia hilo, Mwanga akisema UTT AMIS imekuwa ikitoa elimu kwa makundi mbalimbali juu ya faida ya kuwekeza na kampuni hiyo.



# TANESCO yaagizwa kuongeza umeme vijijini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga ameliagiza Shirika la Umeme nchini (TANESCO) kupeleka umeme mwingi katika vijiji vya Kata ya Mwasauya Jimbo la Singida Kaskazini ili kuwawezesha wananchi kuanzisha viwanda vidogo na kuinua uchumi wao.

Kapinga alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wakazi wa vijiji hivyo vya Mdilu na Mwasauya Wlaya ya Singida katika mkutano wa hadhara baada ya kuwasha umeme wa Mradi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) mzunguko wa pili.

"Meneja wa TANESCO hakikisha suala la kuongeza nguvu ya umeme kwenye vijiji hivi linafanyiwa kazi maana tunataka tupate matajiri wengi kutoka vijijini ambao wataanzisha viwanda vidogo vidogo," alisema.

Naibu Waziri huyo, alitoa agizo hilo kufiatia Mbunge wa jimbo hilo, Ramadhani Ighondo kuwasilisha ombi hilo akisema maeneo mengi ya vijijini wananchi wanashindwa kuwekeza kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo kutokana na nguvu ya umeme kuwa ndogo.

Vilevile, aliagiza TANESCO kupeleka umeme haraka Shule ya Msingi Sokoine iliyopo Kitongoji cha Sokoine na kisima ambacho maji yanasukumwa kwa mashine inayotumia mafuta ya dizeli ambayo ni gharama kubwa. Alisema katika mwaka wa fedha wa 2024/25 serikali imetenga fedha kwa ajili kupeleka umeme kwenye vitongoji 4,000 baada ya kukamilisha kwenye vijiji vyote.

Alisema katika Mkoa wa Singida, miradi ya umeme inayojengwa inagharimu takribani Sh. bilioni 80 na kwamba katika Jimbo la Singida Kaskazini kati ya vijiji 84, vijiji 80 vimefikiwa na umeme na vinne vilivyobaki ifikapo Juni 15, mwaka huu navyo vitakuwa vimepata nishati hiyo.

Meneja wa TANESCO Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Singida, Dodoma na Morogoro, Dastan Ndamugoba, alisema vijiji 437 kati ya 441 vilivyopo Singida vimepata umeme na vilivyobaki vinne ifikapo Juni 16 vitakuwa vimewekewa.

Ndamugoba, alisema pamoja na kwamba lengo la serikali kufikisha umeme kwenye vijiji na vitongoji ni kubadilisha maisha ya wananchi, changamoto iliyopo ni mwitikio mdogo wa wananchi wanaoomba kuunganishiwa kwenye nyumba zao.

"Ni gharama kubwa kuleta umeme huku vijijini na vitongoji, sasa niwasihi wananchi tutumie umeme ili utofauti uonekane kipindi hatuna umeme na sasa. Tutumie fursa hii kuanzisha biashara kama saloon kwa ajili ya kujipatia fedha," alisema.

Meneja Usimamizi REA ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa REA, Romanus Rwena, alisema katika jimbo la Singida Kaskazini kati ya vitongoji 439 ni 275 vimefikishiwa umeme.

Rwena, alisema katika Mkoa wa Singida waliweka lengo la kuwaunganishia umeme wateja 10,000, lakini hadi sasa waliojitokeza ni 4,000.

"Serikali inatumia gharama kubwa sana kuleta umeme, tunaomba maeneo ambako umeme umefika wananchi waunganishwe ili kuleta maendeleo, haitakuwa na maana uwekezaji mkubwa umefanyika halafu umeme hautimiki," alisema.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (wa pili kulia), akikabidhi tuzo maalum kwa Meneja Mkuu wa Taifa Gas Ltd, Devis Deogratius, ikiwa ni ishara ya serikali kutambua juhudi za kampuni hiyo katika utunzaji wa mazingira sambamba na kuunga mkono kampeni ya kumtua mama kuni kichwani inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Mazingira jijini Dodoma juzi. Wengine ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Seleman Jafo (kulia) na Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan 'Zungu'. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Pilikapilika Nanenane kitaifa zaanza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 7.5 kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya kwanza ya Uwanja wa Nanenane jijini Dodoma kwa ajili ya maonyesho ya kitaifa ya kilimo kwa mwaka huu yatakayofanyika mwezi Agosti.

Maonyesho hayo ambayo kila mwaka huanza Agosti moja, yanatarajiwa kufunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kufungwa wakati wa kilele chake Agosti 8 na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema maonyesho hayo yanatarajiwa kuhudhuriwa na watu mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Bashe, alisema awamu ya kwanza ya ujenzi wa uwanja huo itakamilika muda wowote kuanzia sasa.

"Tumeanza ujenzi kwa ajili ya uwanja huo maonyesho yatakuwa mazuri na wakulima watafurahi," alisema Bashe.

Alisema baada ya ujenzi wa uwanja huo kukamilika, watahamia katika viwanja vingine ili kuhakikisha navyo vinaboreshwa.

Alisema mwaka huu maonyesho hayo yatashirikisha wadau kutoka nje na ndani ya nchi kutokana na tija kubwa iliyopo kwa taifa.

Baadhi ya wakulima wameishukuru serikali kwa kuamua kufanya maonyeaho ya kitaifa mkoani hapa huku wakisisitiza maboresho ya uwanja huo yafanyike kikamilifu.

# Mahakama yammwagia sifa Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Profesa Elisante Ole Gabriel, amesifu maboresho yaliyofanywa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan katika muhimili huo kuwa yamesaidia kuendesha mashauri kwa muda mfupi.

Prof. Ole Gabriel alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maboresho yaliyofanya kwenye Mahakama nchini katika kipindi hicho cha uongozi wa Rais Samia.

Alisema maboresho hayo yametokana na uwekezaji mkubwa wa fedha zilizotolewa na Rais Samia kwa idara hiyo.

"Uwekezaji huo umesaidia Mahakama kuendesha shughuli zake kisasa na kuwezesha kutatua mashauri mbalimbali kwa muda mfupi," alisema.

Aliyataja mambo mengine yaliyofanyika katika muda huo kuwa ni pamoja na mahusiano mazuri ya kidiplomasia yaliyofanywa na Rais Samia na mataifa mengine kuheshimisha nchi hususan mahakama.

Alisema pia yameongeza ufanisi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo miundombinu ya majengo, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na ongezeko la watumishi.

Ole Gabriel, alisema msukumo wa pekee ambao serikali imetoa kuiwezesha Mahakama kuwa ni kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kusogeza huduma kwa wananchi.

" Miezi michache baada ya kuingia madarakani, Rais aliahidi serikali itaendelea kuboresha majengo ya mahakama na kuhakikisha kuwa kila mkoa unakuwa na jengo la kisasa la Mahakama Kuu," alisema.

Alisema kwa sasa ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki (IJC) sita unaendelea katika mikoa ya Geita, Katavi, Simiyu, Njombe, Ruvuma na Songwe.

"Maeneo mengine matatu majengo haya yanatarajiwa kuanza kujengwa ni Singida, Lindi na Pemba na makandarasi kwa ajili ya vituo vingine vitatu wameshapatikana na wataanza kazi muda wowote.

Awali alisema katika kipindi hicho cha miaka mitatu, Rais Samia ameongeza idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani kutoka 16 hadi 35 na wa Mahakama Kuu kutoka 76 hadi 105.

Kwa mujibu wa Ole Gabriel, ongezeko hilo limeiwezesha idadi hiyo kuwa na majopo 10 ya vikao vya Mahakama ya Rufani na kupunguza mrundikano wa mashauri katika mahakama hizo.





# Madiwani wagonga ukuta kwa RC

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera amezuia ziara ya mafunzo ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya mpaka halmashauri hiyo itakapopeleka fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mbalizi ili ukamilike na kutoa huduma kwa wananchi.

Homera alizuia ziara hiyo juzi kwenye kikao cha baraza maalumu la madiwani wa halmashauri hiyo cha kusikiliza na kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) baada ya madiwani kuomba ruhusa kwenda kwenye mafunzo, kutokana na ujenzi wa kituo hicho kusuasua kwa kukosa fedha.

Madiwani hao waliomba kwenda kujifunza mambo mbalimbali, ikiwamo utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri ambayo hata hivyo hawakuitaja.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ezekia Soda, alisema 2024 ni miongoni mwa miaka ambayo wamefanikiwa kukusanya mapato kwa asilimia 100, hivyo wanaomba ruhusa ya kwenda kujifunza zaidi kwa wenzao mbinu za kukusanya zaidi mapato.

"Kwa kuwa tumefanikiwa kukusanya vizuri mapato mwaka huu, tunaomba uturuhusu na utusaidie tuende kwa wenzetu ambao wamefanikiwa zaidi ili tukajifunze ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo," alisema Soda. Akijibu ombi hilo, Homera, alisema atawaruhusu madiwani hao, mpaka halmashauri hiyo itakapopeleka fedha za ujenzi wa kituo hicho cha afya.

Mkuu huyo wa mkoa, aliwasisitiza madiwani hao kwamba muda wowote wakipeleka fedha hizo atawaruhusu.

Alisema kituo hicho ni muhimu kwa wananchi wa Mamlaka ya Mji wa Mbalizi ambao wamekuwa wakiongezeka kwa kasi kutokana na shughuli za biashara.

Homera alionyesha kushangazwa kituo hicho kutopelekewa fedha hizo katika mwaka wa fedha uliopita wa 2023/24, hivyo kuzalisha hoja za CAG ambazo hazikuwa na sababu yoyote. "Muwe na huruma na wananchi wa Mbalizi, kile kituo nilikitembelea na niliona umuhimu wake, sasa siwezi kuruhusu ziara yenu mpaka mpeleke fedha pale na ujenzi uendelee, mkipeleka hata leo (juzi) kesho mnaondoka," alisema Homera.

Alisema anataka mpaka kufikia Juni 30 mwaka huu halmashauri hiyo iwe imepeleka Sh. milioni 50 kwenye kituo hicho na mwaka wa fedha ujao zipelekwe tena Sh. milioni 50.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Fredrick Moshi, alisema katika mwaka wa fedha uliopita hawakutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho na badala yake wamepanga kutenga Sh. milioni 50 kwa mwaka ujao wa fedha.

Dk. Moshi, alisema ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 500 na kuhudumia wakazi wa mamlaka ya mji wa Mbalizi na Jirani, hivyo kupunguza msongamano katika hospitali ya wilaya.

Awali Kaimu Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Mbeya, Athuman Seleman, alisema hoja hiyo ilitokana na mipango ya halmashauri hiyo kupeleka Sh. milioni 100 ambayo mpaka sasa haijatekelezwa.



Kamishna Jenerali wa Uhamiaji (CGI), Dk. Anna Makakala (kulia), akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alipowasili mkoani humo jana, kwa ajili ya kuwatunza nishani ya askari wa jeshi hilo, kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mganga mkuu awacharukia wakuu wa vituo

**Elizabeth John,** NJOMBE

WAKUU wa vituo vya afya katika Halmashauri ya Mji Njombe mkoani hapa wameagizwa kufuatilia utoaji huduma wa wataalamu wa afya kwa wananchi na kuhakikisha wanakuwa na mafuta kwa ajili ya gari la wagonjwa.

Agizo hilo lilitolewa na Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Jabir Juma katika kikao kazi cha kujadili taarifa za takwimu za huduma za afya kwa kipindi cha Januari mpaka Aprili mwaka huu katika vituo hivyo.

Dk. Juma aliwaomba kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kusimamia utoaji huduma za afya kwa wananchi ili kunusuru maisha na kuondoa malalamiko miongoni mwao.

"Niwaombe viongozi wote wa vituo vya afya mmepewa mamlaka ya kusimamia wataalamu wa afya katika maeneo yenu nendeni mkatekeleze majukumu kama tulivowaamini, unakuwa kiongozi wa mahali tena wewe mwenyewe unakuwa huwajibiki haileti picha nzuri kwa halmashauri," alisema.

Dk. Juma alivitaka vituo hivyo na zahanati kuhakikisha wanatenga bajeti ya mafuta kwa ajili ya gari la kubebea wagonjwa kwa mwaka ujao wa fesha wa 2024/25.

" Sisi tunatoa huduma kwa wagonjwa wakifika wamezidiwa na wanahitaji msaada wa rufaa ya kwenda hospitali kubwa mnakuwa hamna mafuta," alisema.

Alisema kila kituo kinapaswa kuwa na mafuta ili kusiwe na sababu ya kushindwa kusafirisha wagonjwa kwa kile kinachodaiwa kutokuwapo kwa nishati hiyo.

# Jamii yakumbushwa kuwalinda watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JAMII mkoani hapa imetakiwa kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili, ubakaji na ulawiti ili watimize ndoto ya kupata elimu bora na afya njema.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe Anthony Mtaka wakati wa uwasilishwaji wa taarifa ya awali ya kampeni ya msaada wa kisheria Mama Samia Legal Aid mkoani hapa.

Mtaka aliitaka jamii hiyo kuwa na uwanja mpana wa kuzungumzia maadili na kukumbushana wajibu wa malezi.

Alisema lazima kuwe na nguvu kubwa ya kuzungumzia maadili na kukumbusha wazazi kuwa karibu na watoto.

"Na wajibu huo tufundishane sisi watu wa kizazi chetu wa kike na wakiume kwa sababu madhara haya yanahusu watoto wetu, hawa watu wanaolawiti, hawa watu wanabaka wanatoka kwenye dunia ipi! je tutatengeneza wabakaji na walawitiji wengine?" alihoji Mtaka.

Alisema kampeni hiyo ya msaada wa kisheria imebaini katika suala la malezi kuna mipaka kati ya wazazi na watoto.

"Huenda sisi huku tunajadili mambo mepesi, lakini kizazi kinaharibika hii, kampeni hii ingefanyika hata robo mwaka ili tufikie mikoa mingi zaidi," alisema Mtaka.

Alisema serikali inazo sheria ambazo zimetafsiri kwenye adhabu, kizazi cha sasa kinanafasi ya kuelimisha jamii na kulichukua kwa uzito jambo hilo.

Wakili wa Serikali wa Wizara ya Katiba na Sheria, Daniel Mbaki, alisema katika halmashauri ya mji wa Makambako kuna malalamiko ya kuwepo matukio ya ulawiti na ubakaji hasa kwenye shule moja ya msingi.

"Kuna matatizo makubwa sana kwenye ile shule, lakini masuala hayo tumeawaachia watu wa dawati la jinsia, lakini ilionekana mahusiano kati ya wazazi na watoto yako mbali na hivyo watoto kushindwa kuripoti matukio kwa wazazi wao badala yake wanaenda kwa walimu," alisema Mbaki.

Mkurugenzi wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ya Katiba na Sheria, Emmanuel Mayeji, alisema kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia kwa siku 10 mkoani humo imetekelezwa kwenye kata 71, vijiji na mitaa 221 na kufikia wananchi 66,447, yakiwemo makundi maalumu.

Mayeji alisema katika huduma iliyotolewa na elimu ya sheria, migogoro 550 imewasilisha, kati ya hiyo 229 ni ya ardhi.

# Wajawazito waambukizwa VVU

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJAWAZITO 58 visiwani hapa wamegundulika kuwa na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (UKIMWI) baada ya kupimwa afya katika vituo vya afya.

Takwimu hizo zimetolewa na Waziri wa Afya Nassor Ahmed Mazrui wakati akiwasilisha bajeti ya makadirio na mapato ya wizara hiyo kwa mwaka fedha 2024/2025 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea Chukwani mjini hapa.

Waziri Mazrui alisema kuwa wajawazito hao ni kati ya 46,430 waliojitokeza katika vituo hivyo vya afya kupima afya zao wakati wa kipindi cha ujauzito.

Alisema wajawazito hao kati ya 51,480 waliohudhuria kliniki wakati wa ujauzito 46,430 ni sawa asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 96 ya upimaji wa VVU kwa mwaka 2022/2023.

Alisema wajawazito hao waliogundulika na VVU waliunganishwa kliniki za huduma na tiba kwa wanaoishi na virusi hivyo pamoja na kuanzishiwa dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo.

Mazrui alisema jumla ya watoto 347 waliozaliwa na mama wanaoishi na VVU wamepimwa kwa kutumia mashine ya DNA-PCR na kwamba sita waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU sawa na asilimia 1.7 ikilinganishwa na watoto waliopimwa mwaka 2022/2023 watoto 212 walipimwa VVU na watatu kugundulika na VVU sawa na asilimia 1.4.

Alisema wizara hiyo inaendelea kutoa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kwa kutoa huduma mjumuisho za kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa na Virusi vya Homa ya Ini aina B.

Alisema wajawazito 24,401 wamepimwa kaswende hadi kufikia Machi 2024 kati ya 51,480 waliohudhuria kliniki sawa na asilimia 47 ikilinganishwa na asilimia 59.2 walipimwa ugonjwa huo mwaka 2022/23, kati yao, 42 waligundulika kuwa na maambukizi na kupatiwa matibabu.

"Katika kupambana na maambukizi ya homa ya Ini B wajawazito 19,329 wamepimwa kipimo cha Homa ya Ini B, na mama 108 sawa na asilimia 0.5 walikutwa na maambukizi na tayari wameunganishwa kwenye huduma za matibabu," alisema Mazrui.

Katika kudhibiti maradhi ya kujamiiana, Mazrui, alisema wagonjwa 2,918 wakiwamo wanaume 618 na wanawake 2,300, wamegundulika kuwa na dalili za maradhi ya kujamiiana na kupatiwa matibabu.

Hata hivyo, alisema idadi ya wagonjwa imeshuka kidogo ikilinganishwa na mwaka jana 2,905.

"Mheshimiwa Spika mpaka kufikia mwezi Machi 2024, wateja 1,128, wanaume 1,093 na wanawake 35 wameendelea kutumia dawa kwenye kituo kinachotoa huduma ya "Methadone" katika Hospitali ya Kidongo Chekundu Unguja.

Alisema kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wateja wapya 67 wamesajiliwa na kujiunga na huduma.

Hata hivyo, alisema wizara yake inaendelea kuimarisha huduma katika hospitali na vituo vya afya ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu (SDG 2030) ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia chini ya 70 kwa kila kina mama 100,000, watoto wachanga kufikia 12 kwa kila vizazi hai 1,000 na vya watoto walio chini ya miaka mitano kufikia 25 kwa kila vizazi hai 1,000. Alisema shabaha ya Dira ya maendeleo ya Zanzibar 2050 ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 123 kwa kila mama 100,000 na vya watoto wachanga kufikia 26 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2030.

Hata hivyo, alisema kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wajawazito 41,129 walijifungulia katika vituo vya afya na hospitali Unguja na Pemba kati ya hao, 5,362 kwa njia ya upasuaji.

Alisema wajawazito 41,289 kati ya hao 41,129 walijifungua katika hospitali na vituo vya afya na 160 nyumbani au njia wakati wanapelekwa hospitali na kupatiwa huduma saa 48 baada ya kujifungua.

Kwa upande wa vifo vya watoto chini ya miaka mitano, alisema vimepungua kutoka vifo 56 mwaka 2015 hadi vifo 47 mkwaka 2022 kwa kila vizazi hai 1,000.

Alisema bado kuna changamoto kwa upande wa vifo vya watoto wachanga kwa kuwa mwaka 2015

viliripotiwa 28 katika kila vizazi hai 1,000.

Alisema takwimu zinaonyesha hadi kufikia mwaka 2023 idadi ya vifo vya watoto wachanga bado ni 28 kwa kila vizazi hai 1,000.

Alisema Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza vifo vya watoto hao, ikiwemo kufanya uhakiki ili kujua vyanzo vyake, kuhamasisha elimu ya afya kuhusu lishe, kuhudhuria mapema kliniki kwa mama wajawazito na kufuata ushauri wa wataalamu kuhusu uzazi wa mpango.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoa huduma hospitali binafsi wapewa somo

**Na Mwandishi Wetu**

WATOA huduma wa hospitali binafsi Zanzibar wametakiwa kufuata utaratibu na sheria ziliowekwa na Serikali kupitia Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) ili kuepuka vitendo vya udanganyifu.

Hayo yalisemwa juzi na Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usajili na Usimamizi wa Wanachama, Ali Idrisa Abeid, wakati akifungua kikao cha kujadili changamoto za utoaji wa huduma katika hospitali hizo mjini Zanzibar.

Alisema kuna watoa huduma, wanafanya kazi kinyume na maelekezo waliopewa na ZHSF jambo ambalo linasababisha kuwepo kwa viashiria vya udanganyifu.

Aliwataka watoa huduma hao kuacha kuwaandikia wagonjwa dawa zisizohusiana na maradhi yao kwani kufanya hivyo ni kuwatengenezea usugu wa dawa na kuwasababishia maradhi mengine ikiwamo kufeli kwa figo.

Ofisa Udhibiti Ubora wa Huduma kutoka Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF), Dk. Daud Suleiman Daud aliwataka madaktari hao kutoa elimu kwa wagonjwa wao kabla ya kuwapa matibabu ili kuepuka migongano baina yao.

Alisema endapo madaktari hao watabadilika na kuwa wawazi kwa wagonjwa wao, itawasaidia kuelezea changamoto walizonazo na kuepukana na malumbano na watoa huduma hao.

# Udhalilishaji bado watikisa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya kutokuwapo kwa dhamana na vifungo vya muda mrefu vinavyotolewa dhidi ya wakosaji wa vitendo vya udhalilishaji, hali bado imeendelea kuwa tete juu ya vitendo hivyo nchini.

Hayo yamebainishwa kufuatia ripoti ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliyowasilishwa kwa vyombo vya habari juu ya matukio hayo kwa mwezi Aprili mwaka huu.

Akiwasilisha ripoti hiyo, Mtakwimu Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Asha Mussa Mahfoudh, alisema matokeo 148 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi Aprili.

Alisema waathirika wengi (waathirika 128) walikuwa watoto sawa na asilimia 86.5, wanawake 16 sawa na asilimia 10.8 na wanaume wanne asilimia 2.7.

Alisema miongoni mwa watoto hao, wasichana walikuwa 108 (asilimia 84.4) na wavulana walikuwa 20 (15.6).

Alisema idadi ya matukio kwa mwezi huo yameongezeka kwa asilimia 18.4 kutoka 125 yalioripotiwa Machi huku ubakaji ukiripotiwa kuwa na matokeo 77 ambapo waathirika 70 ni wasichana na saba wanawake.

Aliyataja matukio mengine ni kulawiti (13), kutorosha (7), shambulio la aibu (19) na shambulio (28).

Aliitaja Wilaya ya Magharibi 'A' kuwa inayoongoza kwa matukio hayo 40 sawa na asilimia 27.0, ikifuatiwa na Mjini (34) sawa na asilimia 23.0 huku wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo (1) asilimia 0.7.

Alisema matukio 93 kati ya 148 yaliyoripotiwa, upelelezi wa polisi bado unaendelea.

Alisema majalada 65 yalipokelewa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Aprili 2024 yakihusisha makosa.

Naibu Mrajis Mahakama, Khamis Rashid Khamis, alisema jamii na wazazi wanahitaji kujenga ushirikiano katika malezi ili kuendelea kupunguza vitendo vya udhalilishaji.

Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo la udhalilishaji kukithiri, kuna umuhimu wa jamii kushirikiana ili kumaliza tatizo hilo.

Mrajis kutoka Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali, Khatib Kombo Sheha, alisema ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji ikiwemo ubakaji, jamii inapaswa kuwekeza katika utoaji wa elimu na kuzungumza na watoto namna ya kujilinda.

Mkaguzi wa Polisi Dawati la Jinsia Makao Makuu ya Polisi, Makame Haji Haji, alisema bado jamii inahitaji kuendelea na mapambano dhidi ya vita hivyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**DISMAS BYABATO ISHENGOMA**

anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya SINORAY na TVS zenye usajili namba: MC253 CZB na MC 751 DFV, CHASSIS NAMBA: LD3CK6JXM2009120 na MD625AE30M1K00596 na ENGINE NAMBA: SR162FMJ21059120 na BE3KM1900633. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/109366/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HERI FESTO NUNGWI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya GUTA yenye usajili namba : MC 383 AUN, CHASSIS NAMBA: LAPHDM702F0005327 na ENGINE NAMBA: LB163FML15N05327. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/NJO/NJO/2125/2021**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**HAMIS OMARY ATHUMANI**

anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba: MC 297 BHN, MC 321 BQB, MC 749 BTX, MC 193 CEL, M MC 222 CJE, MC 783 CIX, MC 790 CJX, MC 183 CJY . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KW/94266/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 34 /2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ANASTAZIA CHAHONZA MADWAGO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SESILIA CHARLES MACHINDA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 Mwezi 06 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,
*Marehemu hakuacha wosia
*Futa isioyohusika
Imetolewa leo Tarehe 27 Mwezi 05 Mwaka 2024

..........................................................................
**HAKIMU**

**IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI**
**AT KINONDONI**
**CIVIL CASE NO.25552 OF 2023**
**BANK OF AFRICA.........APPLICANT/PLAINTIFF**
**VERSUS**
**JUDITH BRYSON MASACKY**
**.......RESPONDENT/DEFENDANT**

**TO:**
**JUDITH BRYSON MASACKY**

**NOTICE DATE OF MENTION/HEARING**

THE NOTICE that the above case has been fixed for judgement on 27 day of 06 ..2024 at 8.30am
Before Hon RWEIKIZA
YOU ARE required to appear in this court without failing and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
Given under my Hand and the Seal of the court this 31 day of 05 ..2024.

RESIDENT MAGISTRATE

COPY TO BE SERVED UPON:

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA)**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 961/2024**
**AMICUS TANZANIA LIMITED...MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SUNLIGHT TOURS.......MJIBU MAOMBI NA. 1**
**SUN TRUST CO. LTD......MJIBU MAOMBI NA. 2**

**KWA: SUN TRUST CO. LTD**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la maombi ya madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinapatikana katika Mahakama hii kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 24/06/2024 saa tatu kamili (3:30) asubuhi mbele ya Mhe. Jaji B.K. Phillip kujibu maombi hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

ANGALIA

Kama usipohudhuia siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila ya uwepo wako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 29/05 2024

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa madai Na. 228/2024**
**Jina la Mdai DAS FINANCIAL SERVICES**
**Jina la Mdaiwa SAMWEL C. RICHARD**
**KUITWA SHAURINI**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA: SAMWEL C. RICHARD wa NKUHUNGU**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSH. 7,000,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 11 mwezi 06 mwaka 2024 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithiibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Mhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 05 Mwezi 06 Mwaka 2024.

........................................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HAWA KYAMAN ABDALLAH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0249-0039 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia LORETO GIRLS SECONDARY SCHOOL mwaka 2014 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1599-0568 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia BAOBAB SECONDARY SCHOOL mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/105746/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF ILEMELA DISTRICT**
**AT ILEMELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 12617 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JULIANA KACHUNKWA SHEKANABO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTER OF ADMINISTRATION BY KEMILEMBE VEDASTUS EMANUEL**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

ALL PERSONS CLAIMING TO HAVE ANY INTEREST IN THE ESTATE OF THE ABOVE NAMED DECEASED ARE HEREBY CITED TO COME AND SEE THE PROCEEDING IF THEY THINK FIT BEFORE THE GRANT FOR LETTERS OF AND PROBATE AND ADMINISTRATION IS MADE TO THE ABOVE NAMED PETITIONER.
CAVEAT/OBJECTION TO THE GRANT SHOULD BE FILED ON OR BEFORE 28/06/2024

**DATED AT MWANZA THIS 06/06/2024**
**SENIOR RESIDENT MAGISTRATE**
**ILEMELA – MWANZA**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Putin atishia kushambulia Ulaya

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Valdimir Putin ameonya kwamba nchi yake inaweza kuwapatia mataifa mengine makombora ya masafa marefu kwa ajili ya kushambulia maeneo lengwa ndani ya mataifa ya magharibi.

Putin alisema hatua hiyo itajibu kitendo cha jumuiya ya kujihami ya Ulaya (NATO) kuruhusu Ukraine kutumia silaha zilizotoka kwa wanachama wake kuishambulia Russia.

Kiongozi huyo, pia alithibitisha kwa mara nyingine kuhusu utayari wa kutumia silaha za nyuklia ikiwa kutakuwa na kitisho chochote kwenye eneo lake.

Alisema hatua hiyo ya nchi za magharibi itazidi kudhoofisha usalama wa kimataifa na kuchochea matatizo makubwa kutokana na kuashiria wazi ushiriki wao wa moja kwa moja kwenye vita kati ya nchi yake na Ukraine.

Alisisitiza kuwa wana haki ya kuchukua hatua kama hiyo.

Putin alikuwa akizungumza na waandishi wa habari wa vyombo vya magharibi, jambo ambalo analifanya kwa nadra tangu alipoivamia Ukraine.

Nchi za Marekani na Ujerumani hivi karibuni waliiruhusu Ukraine kutumia makombora ya masafa marefu waliyoipatia kushambulia baadhi ya maeneo ndani ya Russia.

Ofisa mmoja wa magharibi pamoja na seneta wa Marekani walisema Ukraine imetumia silaha walizopewa na taifa hilo kushambulia ndani ya Russia chini ya idhini hiyo inayosimamiwa na Rais Joe Biden.

Katika moja ya masharti Ukraine imetakiwa kutumia silaha hizo ndani ya Russia, lakini kwa kuupigania mji wake wa Kharkiv.

"Kama mtu anadhani inawezekana kupeleka silaha kwenye uwanja wa vita ili kushambulia eneo letu na kutuletea matatizo, kwa nini na sisi hatuna haki ya kupeleka silaha kama hizo kwenye maeneo mengine duniani ambako wanaweza kushambulia maeneo muhimu kwenye mataifa ya magharibi?" alihoji Putin.

"Hilo litakuwa jibu linalowiana. Tutafikiria kuhusu hilo," aliwaambia waandishi hao wa habari.

Rais Putin, ametumia fursa hiyo kurudia kusisitiza kwamba nchi yake haikuanzisha vita dhidi ya Ukraine, na badala yake alipeleka lawama zake kwenye vuguvugu lililoanza mwaka 2014 la wanaounga mkono mataifa ya magharibi

"Kila mmoja anadhani Russia ilianzisha vita nchini Ukraine. Ningependa kusisitiza kwamba si Magharibi wala Ulaya anayetaka kukumbuka namna janga hili lilivyoanza," alisema Putin.

Hata hivyo, Putin alikataa kutaja idadi ya wanajeshi waliokufa kwenye vita hivyo vya miaka miwili, akisema idadi ya vifo vya wanajeshi wa Ukraine ilizidi mara tano ya wale wa Russia.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa NATO, Jens Stoltenberg amezitaka nchi wanachama wahakikishe msaada wa silaha kwa Ukraine haucheleweshwi kama ilivyokuwa mwanzoni mwa mwaka huu.

Wakati wa ziara yake nchini Finland, Stoltenberg alisema Ukraine inahitaji uwajibikaji kutoka kwa washirika wa NATO katika suala la msaada wa kijeshi.

"Katika miezi ya hivi karibuni, tumeona mapungufu, katika utoaji wa msaada wa kijeshi kwa Ukraine. Ni lazima tuhakikishe kwamba hili halitokei tena," Stoltenberg alisema katika mkutano na waandishi wa habari pamoja na Rais wa Finland Alexander Stubb.

Katibu Mkuu wa NATO pia alisisitiza kuwa Muungano huo hauna mpango wa kutuma wanajeshi wake nchini Ukraine.

Rais wa Finland pia alisema kuwa nchi yake haina nia ya kupeleka wanajeshi Ukraine. **DW**

## Israel yaua Wapalestina 35 waliojihifadhi ndani ya shule

**GAZA,** Palestina

IDADI ya watu waliokufa katika shambulio la anga lililofanywa na jeshi la Israel katika shule inayomilikiwa na Umoja wa Mataifa, imeongezeka na kufikia 35 mpaka jana jioni.

Jengo hilo la shule lilikuwa limefurika mamia ya Wapalestina waliokimbia makazi yao katikati mwa mji wa Gaza wakati shambulizi hilo linafanyika.

Waandishi wa habari wa eneo hilo waliiambia BBC kwamba ndege ya kivita ilirusha makombora mawili kwenye madarasa ya ghorofa ya juu ya shule iliyoko katika kambi ya wakimbizi ya Nuseirat.

Video zilionyesha uharibifu na miili ya watu imetapakaa ardhini baada ya tukio hilo.

Jeshi la Israel lilisema lilifanya shambulio hilo kwenye ngome ya Hamas iliyoko katika shule hiyo na kuwaua wapiganaji 20 hadi 30 walioamini walikuwa ndani.

Ofisi ya Vyombo vya Habari vya Serikali ya Gaza inayoendeshwa na Hamas, ilikanusha madai hayo na kuishutumu Israel kwa kufanya mauaji ya kutisha.

Watu waliofariki na kujeruhiwa walikimbizwa katika Hospitali ya Mashahidi ya al-Aqsa, katika mji wa karibu wa Deir al-Balah ambao nao umezidiwa nguvu tangu jeshi la Israel lianze operesheni mpya ya ardhini dhidi ya Hamas katikati mwa Ukanda wa Gaza wiki hii.

Mazingira ya shambulio hilo bado hayajathibitishwa, lakini BBC inajitahidi kuanika ukweli katika siku zinazokuja.

Waandishi wa habari wa eneo hilo na wakazi. **BBC**



Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, akimshika mkono Bernard Duval, ambaye alinusurika katika mauaji yaliyofanywa na majeshi ya Nazi kwenye gereza la Caen mnamo 1944. **PICHA: AP**

## Odinga ashangaa serikali kumuunga mkono

**NAIROBI,** Kenya

KIONGOZI wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, ameshangazwa na hatua ya serikali ya nchi hiyo kumuunga mkono katika nia yake ya kuwania uenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika.

Odinga alikaribisha hatua hiyo ya serikali ya kuunda kamati itakayoshirikiana na timu yake kwa ajili ya kufanikisha kampeni za kushawishi mataifa ya Afrika kumchagua.

"Nilishangazwa serikali ya Kenya kuniunga mkono, nilitarajia wao watasema hapana, sijui mbona walikubali ni uamuzi wao, sio wangu." Alisema Raila Odinga.

Waziri wa Mambo ya Nje ambaye ni mkuu wa mawaziri nchini humo, Musalia Mudavadi, alisema kamati ya serikali itamfanyia kampeni Odinga, na kwamba serikali ya nchi hiyo inaunga mkono azma yake.

"Tulikubali kumuunga mkono kwa maana Raila ana uwezo, na tunaangazia maslahi ya Kenya kitaifa, pamoja na ya Afrika. Kwa hivyo hili halihusiani na siasa zetu, na itakuwa fursa kwa Kenya kuchukua uongozi katika bara letu, na Raila Amollo Odinga ana tajiriba ya kutosha." Alisema Mudavadi.

# SIMBA QUEENS YATAMBA ITATANGAZA UBINGWA LEO

**Na Somoe Ng'itu**

BINGWA mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania huenda akajulikana leo endapo vinara wa ligi hiyo, Simba Queens watapata ushindi au sare yoyote leo watakaposhuka ugenini kuikabili Alliance Girls kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Simba Queens wanaongoza katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 43 wakifuatiwa na wapinzani wao wa karibu mabingwa watetezi, JKT Queens yenye pointi 34, kila timu imebakisha mechi tatu ili kumaliza msimu.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' alisema kikosi chake kiko imara na kimejipanga vizuri kuwakabili wapinzani wao.

**Mgosi alisema mechi zote za ligi zina ushindani na wao hawatarajii kupata ushindi kirahisi.**

"Kila kitu kiko vizuri kuelekea kurudisha kombe letu," alisema kwa kifupi Mgosi, straika wa zamani wa Simba na DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Aliongeza wachezaji wake wote wako katika hali nzuri na wanachosubiri ni muda wa mchezo kufika.

"Ninahitaji kupata ushindi katika michezo yote iliyosalia ili kufikia malengo. Pia tunajua hakuna mechi rahisi, hatutabweteka, nimewaambia wachezaji waongeze umakini," Mgosi alisema.

Mbali na vita ya kusaka ubingwa, straika wa Simba Queens, Aisha Mnuka na Stumai Abdallah wa JKT Queens, wanachuana vikali kuwania kiatu cha dhahabu katika ligi hiyo.

Kwa sasa Aisha anaongoza akiwa ametikisa nyavu mara 18 akifuatiwa Stumai mwenye magoli 16.

"Malengo yangu ni kuisaidia timu yangu kufikia malengo, lakini nina mpango wa kutwaa tuzo ya mfungaji bora msimu huu. Najua si kazi rahisi, nitapambana kuhakikisha nafikia malengo," Aisha alisema.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Bunda Queens itakayowavaa Yanga Princess wakati Baobab Queens itawaalika Ceasiaa huku JKT Queens ikicheza dhidi ya Fountain Gate.

## *Pamba Jiji yamfuata Kopunovic*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba Jiji ya Mwanza ipo katika mazungumzo na kocha wa zamani wa Simba na Tabora United, Goran Kopunovic kwa ajili ya kuinoa timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Pamba Jiji imerejea Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuikosa kwa miaka 23, tayari imenza maboresho ya kikosi chake kwa kuongeza nguvu kwenye benchi la ufundi.

Habari kutoka ndani ya Pamba Jiji zinasema, pia mabosi wa timu hiyo wanafanya mazungumzo na Kocha, Mbwana Makata, ambaye aliwapandisha ili kubakia kama Kocha Msaidizi.

"Mazungumzo na Kopunovic yamefikia mahali pazuri, yakikamilika atachukua nafasi ya Makata, kuna mgawanyiko, baadhi ya viongozi wanataka abaki kama kocha msaidizi, wengine wanasema waachane naye, lakini hii itazingatia uamuzi wake mwenyewe kama anaweza kubaki au kuondoka," kilisema chanzo chetu.

Kuhusu usajili, taarifa zinasema tayari mchakato wa kusajili wachezaji wenye vipaji na uzoefu unaendelea na wanataka timu yao icheze soka la ushindani.

"Tutasajili wachezaji wakubwa na wenye uzoefu na Ligi Kuu, hilo halipingiki, lakini pia tutakuwa na vijana wenye vipaji kutoka ukanda huu ambao naamini watatikisa soka la Bongo kama ilivyokuwa enzi zetu," alisema.



Nahodha wa Twiga Stars, Oppah Clement (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Sudan Kusini katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam wiki iliyopita. Twiga Stars ilishinda mabao 3-0. **PICHA: TFF**

## Ushirikina watajwa maoni Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu imeanza kupokea maoni kwa ajili ya maboresho ya Kanuni za Ligi Kuu Tanzania Bara za msimu mpya wa 2024/25, huku wadau wengi wakionekana kutaka adhabu kali zichukuliwe kwa timu itakaobainika kufanya vitendo vya kishirikina viwanjani.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, alisema tayari wameshaanza kupokea maoni kwa njia mbalimbali za mawasiliano na wanaahidi pia watawatembelea wadau wa soka nchini vikiwamo vyombo vya habari.

"Tumeanza kupokea maoni, lakini ukweli kabisa nikiri kanuni iliyovunjwa sana msimu huu ni ile inayozungumzia imani za kishirikina, na ndiyo inayotolewa maoni mengi kwa sasa na wadau kuliko zingine, kuonyesha ni namna gani hawaridhishwi na adhabu zinazotolewa, wanasema iliyopo haizuii au haiwatishi watu kuendelea na tabia hiyo," alisema Boimanda.

Amewataka wadau kuendelea kutoka maoni kwa sababu yatasaidia kuiboresha ligi ambayo inazidi kufanya vyema hapa barani Afrika.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Steven Mguto, alisema kuelekea msimu ujao wanafikiria kupeleka mapendekezo ya timu itakayobainika kufanya vitendo vya ushirikina ikatwe pointi, badala ya faini au vyote kwa pamoja.

## Inter Zanzibar FC kushiriki Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Inter Zanzibar FC, Abdulrahman Mohamed, amesema haikuwa kazi rahisi kuipandisha timu hiyo ambayo msimu ujao itashiriki Ligi Kuu Zanzibar.

Inter Zanzibar imefanikiwa kupanda daraja baada ya kuwafunga Paje Star FC mabao 2-1 katika mchezo wa fainali ya kwanza ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Kocha huyo alisema anafuraha kuona wametimiza lengo baada ya kupambana katika ligi hiyo iliyokuwa ngumu na ilishirikisha timu zenye uzoefu.

"Hatukukata tamaa kwa kila matokeo tuliyokuwa tunapata katika mzunguko wa kwanza. Timu ilijidhatiti zaidi kipindi cha pili na kurekebisha makosa yote jambo lilopelekea kutopoteza mechi hata mmoja katika michezo tisa waliyocheza," alisema kocha huyo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Said Suleiman, alisema ligi ilikuwa ngumu na yenye ushindani lakini nidhamu nzuri ya wachezaji na kujituma ndio siri ya kupata mafanikio.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALISON KUTUA SAUDIA

KIPA wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Brazil, Alisson mwenye umri wa miaka 31, ametambuliwa na Saudi Pro League kama mmoja wa walengwa wao wakuu msimu huu wa joto. ***(Teamtalk)***

### BARKLEY NJIA MOJA

KLABU ya Aston Villa inajipanga kukamilisha dili la pauni milioni tano kwa ajili ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Ross Barkley, mwenye umri wa miaka 30, kutoka Luton Town. ***(talkSPORT)***

### NKETIAH KURUHUSIWA

ARSENAL itamruhusu mchezaji wa kimataifa wa Uingereza, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 25, kuondoka katika klabu hiyo, ingawa kwa shingo upande huku Fulham wakiwa tayari kutoa karibu pauni milioni 30 kwa ajili ya fowadi huyo, ambaye pia anazivutia Crystal Palace, Wolves na Everton ***(Sun)***

### ZINCHENKO NA ARSENAL

ARSENAL pia iko tayari kutoa ofa kwa beki wa kushoto wa Ukraine, Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akihusishwa na Bayern Munich. ***(Football Insider)***

### SUMMERVILLE AWINDWA

WINGA wa Leeds United Mholanzi Crysencio Summerville ameonekana kuwindwa na Liverpool kwa pauni milioni 30.***(Mirror)***

### BELLINGHAM AGEUKA LULU

KLABU ya Sinderland imedhamiria kutomuuza mchezaji wa kimataifa wa Uingereza Jobe Bellingham, mwenye umri wa miaka 18, huku Tottenham, Brentford na Crystal Palace zikimhitaji kiungo huyo. ***(Guardian)***

### INACIO ATAKIWA ENGLAND

KLABU za Manchester United na Liverpool zinamfuatilia beki wa kati wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Goncalo Inacio, mwenye umri wa miaka 22. ***(Fabrizio Romano)***

### SANCHO KUIBANA UNITED

WINGA wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24, atashinikiza kurejea Borussia Dortmund kwa mkataba wa kudumu kutoka Manchester United msimu huu. ***(Star)***

### JOSELU MAMBO SAFI

REAL Madrid wameamua kutumia chaguo lao kumsajili fowadi wa Hispania, Joselu mwenye umri wa miaka 34, kwa mkataba wa kudumu kutoka Espanyol. ***(The Athletic)***

### ENDO ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanapanga kumsajili kiungo mpya, huku nyota huyo wa kimataifa wa Japan, Wataru Endo, mwenye umri wa miaka 31, akitazamwa kama mchezaji wa kushikilia nafasi hiyo kwa muda tu. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND AFANYA SIRI MKATABA WAKE CITY

**MANCHESTER,** England

**Lakini akiri amekuwa na miaka miwili ya kupendeza huku...**

ERLING Haaland amekataa kueleza iwapo mazungumzo ya kusaini mkataba mpya yanaendelea huko Manchester City, baada ya kufurahia msimu mwingine kileleni mwa Ligi Kuu England.

**Tangu kuhamia England msimu wa joto wa 2022, Haaland amekuwa mfungaji bora zaidi, na kuisaidia City kushinda mataji muhimu.**

Pia amefurahia kampeni zilizozaa matunda katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, na alikuwa mchezaji bora wakati wa msimu wa 2022/23.

Raia huyo wa Norway mkataba wake wa sasa utamalizika ifikapo mwaka, 2027 lakini amekataa kuzungumza juu ya uwezekano wa kuongeza muda wake wa kukaa hapo Etihad.

Akizungumza na tv2, Haaland alikuwa mwepesi wa kukataa hilo, akisema: "Nimekuwa na miaka miwili ya kupendeza, na nina miaka mitatu iliyobaki. Hiyo ndiyo tu ninaweza kusema."

Wakala wa Haaland, Rafaela Pimenta, ambaye alichukua usukani kufuatia kifo cha Mino Raiola, mnamo 2022, ameweka maelezo kamili ya mkataba wa mchezaji huyo kuwa siri.

Hata hivyo, Pimenta alisema hadharani wateja wake wote wana kifungu cha kuachiliwa ili kuwaweka katika udhibiti wa hatima yao.

Haaland pia alitoa maoni kuhusu Pep Guardiola, ambaye amefanya kazi chini yake tangu awasili.

"Ni kweli natumaini atakaa kwa muda mrefu, lakini kwa vyovyote vile City ni klabu ambayo itakuwa na mmoja wa makocha bora bila kujali, kabla na baada ya enzi za Pep, kwa hiyo siku akiacha kazi nina uhakika kocha imara ataingia," Haaland alisema.

Huku msimu wa soka ukiwa umekamilika, wachezaji wengi wamejiunga na timu zao za taifa kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya Euro 2024 na Copa America.

Haya hivyo, Haaland atalazimika kuwatazama wachezaji wenzake wa City kutoka mbali, baada ya Norway kushindwa kufuzu mashindano ya Euro 2024.

Lakini juhudi zake katika ngazi ya klabu haziwezi kuwa na dosari, huku mshambuliaji huyo akitwaa taji lingine la Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England kwa msimu wa 2023/24.

Mashabiki walikuwa wepesi kutoa maoni yao kuhusu kushuka kwa kiwango chake wakati wa kampeni za hivi punde, lakini bado Haaland alishinda mbio za kuwania taji la mfungaji bora, akifunga mabao 27 katika mechi 31 za Ligi Kuu England.



# PSG YAZUIA MSHAHARA NA BONASI ZA MBAPPÉ

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imeripotiwa kutomlipa, Kylian Mbappe, mshahara wa Aprili na Mei, mwaka huu pamoja na bonasi ya Februari ambayo ni zaidi ya Euro milioni 70.

Mbappe amekuwa na kutokueleewana na mabosi wake wa zamani, PSG baada ya kuondoka kwa uhamisho wa bure, na ili kufidia hasara za kumpoteza mchezaji huyo bila malipo, PSG wamezuia karibu Euro milioni 70 katika mishahara yake.

Mbappe kwa sasa yuko Metz na kikosi cha Ufaransa kinachojiandaa kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Euro 2024.

Lakini alipoulizwa kuhusu jinsi mwaka wake wa mwisho PSG ulivyoisha, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alisema;

"Walinifanya nielewe sitacheza tena PSG, kwenye klabu waliniona nina kiburi.

"Mimi huwa nasema niliyopitia sitatamani mtu yeyote apitie hivyo naona haifai kuja kulalamika nikiona kinachoendelea kuna mambo mabaya duniani."



# Neymar ampa Vinicius Junior Ballon d'Or

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

MCHEZAJI wa Al Hilal ya Saudi Arabia, Neymar Jr, ameweka wazi kumuunga mkono mbrazili mwenzake, Vinicius Junior anayekipiga Real Madrid ndiye atakayeshinda tuzo ya Ballon d'Or kwa mwaka huu.

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid amefurahia msimu mwingine mzuri zaidi, akishinda mataji ya Uefa na La Liga.

Alifunga bao katika mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Los Blancos walipoizamisha Borussia Dortmund mabao 2-0.

Hilo limemfanya Neymar kudai mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 hakika atatawazwa kuwa mchezaji bora wa mwaka 2024.

Kwa sababu hiyo Neymar anaamini Vinicius Junior amekuwa mchezaji bora wa dunia mwaka 2024 - hivyo anastahili kushinda Ballon d'Or.

Neymar anaamini Vini ataiongoza vyema Brazili katika michuano ya Copa America msimu huu wa joto na kutwaa ubingwa wa kombe hilo.

Vinicius alifunga mabao sita katika Ligi ya Mabingwa msimu huu, na hivyo akatajwa kuwa mchezaji bora wa mashindano hayo kwa msimu wa mwaka 2023/24.

Pia alichaguliwa katika timu bora ya La Liga baada ya kuisaidia Real Madrid kutwaa taji la Hispania.

# Conte kocha mpya Napoli

**NAPLES,** Italia

ANTONIO Conte amethibitishwa kuwa kocha mkuu mpya wa Napoli.

Mtaliano huyo amepata kibarua hicho ikiwa imepita zaidi ya mwaka mmoja tangu alipotimuliwa Tottenham Hotspur na anarejea kufanya kazi nyumbani kwao kwa mara ya kwanza tangu 2021, alipoondoka Inter baada ya kushinda taji lao la kwanza la Serie A ndani ya miaka 11.

Conte alihusishwa na klabu za Bayern Munich, Milan na Chelsea, lakini sasa amekamilisha kurejea kwenye uongozi na Napoli.

"Napoli ni mahali pa umuhimu. Nina furaha na kufurahishwa na wazo la kukaa kwenye benchi la bluu. Hakika ninaweza kuahidi jambo moja: Nitafanya niwezavyo kwa ajili ya ukuaji wa timu na klabu. Kujitolea kwangu, pamoja na wafanyakazi wangu," alisema Conte.

Baada ya kushinda Scudetto yao ya kwanza katika kipindi cha miaka 23 chini ya uongozi wa Luciano Spalletti mnamo 2023, kabla ya kuondoka Italia, Napoli iliendelea kupitia makocha watatu msimu uliofuata na kumaliza nafasi ya chini ya 10 katika Serie A.

Sasa wamemgeukia Conte, ambaye anajiunga na klabu ya saba ya Italia katika maisha yake ya ukocha, kusaidia kufufua mafanikio yao.

Conte atatafuta kujenga upya heshima yake baada ya kuondoka Spurs Machi, 2023 kwa hali mbaya.



# AZAM YAJIPANGA KUWEKA HISTORIA MASHINDANO CAF

**Na Adam Fungamwango**

MABOSI wa Azam FC wamesema tayari wameanza maandalizi kuhakikisha timu yao inatinga hatua ya makundi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki msimu ujao.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Azam FC, Thabit Zacharia, aliliambia gazeti hili jana, moja ya maandalizi wamefanya na yamekamilika ni usajili wa wachezaji huku mikakati mingine ikiendelea vyema.

Zacharia alisema watahakikisha wanapambana ili kufikia malengo ya kufika hatua ya makundi kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo.

"Lengo letu ni angalau tufike hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na tukishafika huko mambo yanaweza kubadilika kulingana na hali itakavyokuwa, lakini kikubwa tufike na ndiyo jambo limetuumiza miaka mingi, kwa maandalizi tutakayofanya na uwezo wa Mungu safari hii tutafika," alisema ofisa huyo.

Aliongeza wanaendelea vyema na mpango namba moja wa kusajili wachezaji wenye hadhi ya kucheza michuano hiyo ya kimataifa na unaendelea kutekelezeka kwa kiwango cha juu.

**"Tumefanya usajili mapema kwa sababu tulikuwa tunajiandaa na michuano ya kimataifa. Tulijua kama hatukupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, basi tutakwenda kucheza Kombe la Shirikisho.**

Na hata usajili wenyewe unaona tuliufanya kwa wachezaji wenye hadhi ya kimataifa ili kutukwamua pale ambapo tulikuwa tukikwama kila mwaka," Zakaria alisema.

Tayari Azam imeshatanga kuwanasa wachezaji wanne, beki wa kati, Yoro Mamadou Diaby na kiungo mshambuliaji Franck Tiesse, wote kutoka Stade Malien ya Mali lakini pia wakimsajili raia wa Colombia wawili, Jhonier Blanco kutoka Aguilas Doradas ya Rionegro na kiungo mshambuliaji, Ever Meza kutoka Leonnes pia ya huko.

Azam FC ilimaliza msimu uliopita katika nafasi ya pili nyuma ya mabingwa, Yanga lakini ikifungwa na timu hiyo ya Jangwani katika fainali ya FA.



Mchezaji wa Yanga Princess akifanya mazoezi kabla ya kuanza safari kuelekea mkoani Mara kuwafuata wenyeji Bunda Queens kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Karume ulioko Musoma. **PICHA: MTANDAO**

## Aziz Ki aendeleza sintofahamu

INATOKA UKURASA 24

kumalizana naye hivi karibuni.

"Ukiwa unaendesha soka kuna mambo yanajitokeza, kuna wachezaji wanakuja lakini wanashindwa kukupa kile unachotarajia, Hafiz ni kweli tulimwondoa kwenda klabu nyingine lakini tulipaswa tumlipe kiasi fulani cha fedha ili tumalizane naye, kuna kuchelewa kidogo katika malipo hayo.

Tutamlipa, uongozi wa Yanga siku za karibuni ulikuwa umelenga zaidi shughuli za kumaliza msimu, ajenda ya kumaliza madeni kwa wachezaji wote wanaotudai itafanyiwa kazi ndani ya siku tatu hizi ili twende dirisha la usajili kila kitu kikiwa kimekamilika," Kamwe aliongeza.

Wakati huo huo, Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), limetangaza kuiondolea Yanga adhabu ya kufungiwa kusajili wachezaji baada ya kurekebisha upungufu uliojitokeza katika uhamisho wa mchezaji ambaye hakutajwa jina lake.

Yanga inatajwa haikuingiza uthibitisho wa malipo ya uhamisho wa mchezaji husika katika mfumo wa usajili (TMS), licha ya kukumbushwa kufanya hivyo.

Hata hivyo shirikisho hilo limesema Yanga bado ina adhabu nyingine ya kufungiwa kusajili baada ya kushindwa kumalizana vyema na mchezaji wake, Lazarus Kambole, ambaye alifungua kesi ya madai ya malimbikizo ya mishahara na kuvunja mkataba bila ya kufuata taratibu.

## Simba SC yatamba itarejesha heshima

INATOKA UKURASA 24

ndani ya timu yetu, mazungumzo yanaendelea kupitia mawakala na watu wetu wanaosaka nyota, utakuwa usajili wa kishindo," aliongeza.

Wakati huo huo, Simba imetangaza nafasi ya kazi kwa nafasi ya Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki na mwisho wa kutuma maombi imetajwa kuwa ni Juni 14, mwaka huu.

Taarifa imesema mwombaji anatakiwa lazima awe mwanachama wa Simba na mwenye umri usiozidi miaka 50.

## *Taifa Stars kuifuata Zambia kesho*

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), itaondoka nchini kesho kuelekea Zambia kwa ajili ya kucheza mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2026.

Zambia maarufu Chipolopolo itaikaribisha Taifa Stars katika mechi ya Kundi E itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko katika Mji wa Ndola.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema jana kikosi cha timu hiyo kimekamilika baada ya nyota ambao walikuwa katika majukumu ya klabu zao kuripoti.

"Kikosi cha Stars sasa kimekamilika, wachezaji wote walioitwa wamewasili, na leo (jana), wamefanya mazoezi kwa Mkapa na kesho (leo), wataendelea kujinoa hapo, wanajiimarisha kwa ajili ya kuhakikisha wanapata matokeo bora huko Zambia," alisema Ndimbo.

Aliongeza benchi la ufundi la Stars lililoko chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Hemed Morocco, limesema limeridhishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji katika michezo ya kirafiki iliyofanyika Indonesia wiki iliyopita.

Tanzania inaburuza mkia katika Kundi E ikiwa na pointi tatu sawa na vinara Morocco, Zambia na Niger, hii inatokana na tofauti na mabao ya kufunga na kufungwa.

Michezo
Ijumaa Juni 7, 2024
Nipashe



Haaland afanya siri mkataba City UKURASA 21

# Aziz Ki aendeleza sintofahamu Yanga SC

## Hata hivyo mabosi waahidi kuanika mikakati ya msimu mpya Jumapili...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki, akiandika waraka maalumu wa kuwashukuru wachezaji, viongozi, mashabiki na wafanyakazi wote wa timu hiyo kwa ushirikiano waliompa, klabu hiyo inatarajia kutangaza mikakati yake kuelekea msimu mpya kwenye mkutano mkuu wa wanachama utakaofanyika keshokutwa jijini Dar es Salaam.

**Hata hivyo, Aziz Ki alifuta waraka huo uliongeza taharuki kwa mashabiki na wanachama wa Yanga muda mfupi baada ya kuuandika katika akaunti yake ya Instagram.**

Aziz Ki ameendelea na sintofahamu kuhusiana na hatima yake baada ya kushindwa kutia saini mkataba mpya wa kuwatumikia mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mabosi wa Yanga wamesema wanatarajia kujiimarisha kwa lengo la kupata mafanikio zaidi katika msimu mpya wa mashindano na hawakuwa tayari kuzungumzia andiko hilo la Aziz Ki, nyota raia wa Burkina Faso.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi ya mkutano huo yanaendelea vyema na amewataka washiriki waliotajwa kwenye katiba yao ambao ni viongozi watano wa kila tawi kuhudhuria bila kukosa.

"Tuko katika maandalizi ya kuelekea mkutano wetu utakaofanyika Jumapili, huu ni Mkutano Mkuu wa Wanachama wa kikatiba, lakini hawahushiriki wote, wale viongozi ambao katiba inawatambua, ni viongozi watano kutoka kwenye kila tawi duniani kote ambako matawi ya Yanga wanapatikana.

Tunaamini viongozi wote wa matawi watakuja kwa wingi na utaongozwa na Rais Hersi Said, kila msimu ukimalizika ni lazima aje awaambie wanachama msimu ulivyokuwa na yale ambayo walimwagiza akayatekeleze kama kiongozi wao ameyatekeleza kwa asilimia ngapi, baada ya hapo kama wataafiki, tunakuja kupanga pamoja kuelekea msimu unaofuatia," alisema Kamwe.

Aliongeza pamoja na mafanikio waliyopata msimu huu, Hersi atabainisha mikakati ambayo itaifanya klabu na timu yao kuwa imara zaidi na tishio Afrika katika msimu ujao wa mashindano.



Kuhusu Hafiz Konkoni, ambaye kwa sasa anakipiga kwa mkopo katika timu ya Dogan Turk Birligi ya Cyprus, akitokea Yanga, alisema ni kweli anaidai fedha Yanga na wanajipanga

INAENDELEA UKURASA 23



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Simon Msuva (kushoto), akimtoka kiungo wa timu hiyo, Mudathir Yahaya, katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Kundi E ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Zambia itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola. **PICHA: TFF**

# Simba yatamba itarejesha heshima

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU bado ikiwa katika mchakato wa kusaka kocha mpya atakayerithi mikoba ya Abdelhak Benchikha, uongozi wa Simba umesema unajipanga kurejesha katika makali na heshima waliyokuwa nayo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Simba imemaliza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita katika nafasi ya tatu, ikitolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya robo fainali na ikiiaga michuano ya Kombe la FA hatua ya 16 bora.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili uongozi wa klabu hiyo hautaki kurudia makosa na wanaamini kila idara iliyokuwa na mapungufu itafanyiwa kazi.

Ahmed alisema wanaamini mikakati na mipango inayofanywa na viongozi wao itaifanya timu hiyo kuwa na makali yaliyozoeleka na kuipa sifa Tanzania.

"Nasema hivi, Simba tutarudi kwa kishindo msimu ujao kutokana na aina ya usajili tunaokwenda kuufanya. Kila kitu kitarudi katika mstari, tuliteleza, lakini hatujaanguka, tunawaambia hao, wajipange," alisema Ahmed.

Alisema wanafahamu hakuna mwanachama au shabiki ambaye meridhishwa na kilichotokea msimu uliomalizika na hivyo ndio sababu kubwa ya kufanya maboresho.

"Usajili utakaofanyika safari hii utakuwa mkubwa, tumedhamiria na tumejipanga kuhakikisha tunakuwa imara, ninaamini tutarudisha heshima yetu tuliyokuwa nayo, iliyozoeleka.

Tunaomba mashabiki wetu wawe na subira, tutasajili wachezaji wazoefu na ambao wataleta ushindani katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya CAF,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >